SportPesa
TZS. 735,865,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



KESI YA MBOWE
**Komandoo** mwingine adai kuteswa polisi
UKURASA 3




**Ronaldo: Sishindani na Messi tuzo Ballon d'Or**
UKURASA 21


# Nipashe

**Alhamisi Desemba 2, 2021** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580782

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Maambukizi mapya VVU vijana yatisha

• **Asilimia** 40 wa miaka 15- 24, wasichana watajwa kuwa vinara kwa asilimia 80... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**
**TANZANIA YAVINADI VIVUTIO VYA UTALII MKUTANO KIMATAIFA**
TANZANIA inashiriki Mkutano Mkuu wa 24 wa Kimataifa wa Utalii Duniani...

**UKURASA WA 5**
**KADA ATANGAZA NIA ACT KUMRITHI MAALIM SEIF**
KADA wa Chama cha ACT-Wazalendo, Hamad Masoud Hamad, ametangaza...

**UKURASA WA 7**
**TANAPA YACHUKUA HATUA WANYAMAPORI WALIOZAMA TOPENI**
SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limekiri baadhi ya wanyamapori...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimsikiliza Aisha Hassan (kushoto), alipotembelea banda la kundi la Timiza Malengo linalofadhiliwa na Asasi ya Vijana Tanzania (TAYOA), katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani jijini Mbeya, jana. Watatu kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenista Mhagama. **PICHA: OWM**

## TMA yaonya ongezeko mvua Dar, Kaskazini

UKURASA 3




Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa kati wa Benki ya CRDB, Boma Raballa (katikati), akionyesha aina mpya ya kadi za 'TemboCard', wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Tisha na TemboCard Visa, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Idara wa Masoko wa benki hiyo, Joseline Kamuhanda na Kaimu Meneja Mwandamizi wa Biashara ya Kadi, Erica Mwaipopo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Shahidi wa kesi ya Ole Sabaya ageuziwa kibao

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YALIA RATIBA, YANGA SIRI YA MABAO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (katikati), akiwa na Balozi wa Tanzania nchini Hispania mwenye makazi yake ya kudumu nchini Ufaransa, Samwel Shelukindo (kulia) na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utalii, Richie Wandwi (kushoto), wakiwasili kwa ajili ya kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa 24 wa Shirika la Umoja wa Kimataifa linaloshughulikia Masuala ya Utalii Duniani (UNWTO), ulioanza jijini Madrid, Hispania jana. **PICHA: WMU**

# Maambukizi mapya VVU vijana yatisha

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MAAMBUKIZI mapya kwa vijana kati ya miaka 15 hadi 24 yamezidi kuongezeka huku wasichana wakiwa vinara katika janga hilo, imebainika.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Ajira, Uratibu wa Bunge, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini hapa.

Mhagama alisema taarifa za utafiti zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ya VVU yanawakabili zaidi vijana wenye umri huo na kwamba yamefikia asilimia 40 huku asilimia 80 kati ya hao ni vijana wakike jambo ambalo ni hatari kwa nguvu kazi ya taifa.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ukiwamo wa kudhibiti Ukimwi wa mwaka 2018/19 na 2022/23. Mpango huo unalenga kupunguza maambukizi mapya ya VVU, kupunguza vifo vitokanavyo na VVU na kuhakikisha watu wanaoishi na maambukizi ya VVU wanaendelea kutumia dawa.

Waziri Mhagama alisema kwenye mkakati huo, serikali imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji ikiwa ni pamoja na kubadili tabia kwa vijana ili kudhibiti maambukizi mapya.

"Lakini pia tuna mipango maalumu ya kudhibiti maambukizi kwenye mikoa ambayo ina maambukizi makubwa ambayo yako juu ya kiwango cha kitaifa ikiwamo Njombe, Iringa, Mbeya, Kagera na Geita ambayo ipo juu ya kiwango cha kitaifa," alisema Mhagama.

Alisema kwa sasa kuna baadhi ya mikoa ambayo imebainika kuwa na kasi kubwa ya maambukizi ikiwamo Geita, Simiyu, Manyara na Dodoma.

Pia alisema serikali ina mipango maalumu ya kudhibiti maambukizi mapya kwenye maeneo yenye shughuli maalumu za uzalishaji kama vile migodi na uvuvi kwa kusambaza kondomu pamoja na kutoa elimu ya kujikinga.

**WANAOVUJISHA SIRI WAONYWA**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ambaye alikuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan aliziagiza mamlaka zinazohusika kuwachukulia hatua za kisheria watumishi wa afya wanaovujisha siri za watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) wanaokwenda kupata huduma kwenye vituo vya afya kwa kuwa ni kinyume cha maadili ya kazi yao.

Pia aliagiza vyombo vya sheria kuwachukulia hatua kali watu wote wanaoendeleza vitendo vya unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU kwa kuwa vitendo hivyo vinasababisha watu kuogopa kupima na kutumia dawa.

Alisema vitendo hivyo vya unyanyapaa na uvujishaji wa taarifa za watu wanaoishi na maambukizi ya VVU, vinakwaza na kufifisha juhudi za serikali na wadau kupambana na janga hilo la Ukimwi.

"Vitendo na kauli za unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU vinavyoendelea hasa maeneo ya vijijini havikubaliki. Naagiza mamlaka zinazohusika kuchukua hatua dhidi ya watu wanaoendeleza vitendo hivyo," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu alisema Tanzania imekuwa ikipambana na maambukizi ya VVU kwa muda wa miaka 38 na kwamba kutokana na mapambano hayo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu namna ya kujikinga na maradhi hayo.

## Mwanafunzi abakwa, auawa na hatimaye akitobolewa macho

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Maendeleo Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Zinati Alifa (13), amebakwa, kuuawa kisha maiti yake kutupwa kwenye mapango ya miamba ya Mto Kabomola.

Aidha, mwili wa mwanafunzi huyo ambaye ni mkazi wa mtaa wa Mchema Kata ya Mkomaindo, ulikutwa umetobolewa macho na kitu chenye ncha kali. Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mchema, Shaibu Chande, alisema mwili huo uliokotwa juzi ukiwa umefichwa kwenye miamba hiyo.

Alisema kabla ya kufikwa na umauti, mwanafunzi huyo Septemba 26, mwaka huu majira ya saa 11:30 jioni aliwaaga wazazi wake kuwa anakwenda kuokota korosho na maembe kwenye mashamba yaliyopo eneo la Mchemba kilomita chache kutoka kwao.

"Mwanafunzi huyo hakurejea hadi usiku ndugu walihofia usalama wake na kuanza kumtafuta bila mafanikio kwa kuwa haikuwa tabia yake. Walikwenda hadi kwenye shamba ambalo aliaga anakwenda na hawakumpata," alisema.

Kwa mujibu wa Chande, Septemba 27, wanafamilia wakishirikiana na jamii walimtafuta maeneo mbalimbali na hawakumpata.

Alisema baada ya kumkosa kwa siku mbili, walitoa taarifa Serikali ya Mtaa na Kituo cha Polisi Wilaya ya Msasi.

Chande alisema ofisi ya serikali ya mtaa wa Mchema jana majira ya saa 9:00 jioni ilipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema pamoja na wanafamilia kuwa mwili wa mwanafunzi huyo umeokotwa maeneo ya miamba ya milima ya eneo la Kabomola ukiwa umesokomezwa kwenye makorongo ya miamba hiyo.

Alisema kutokana na hali ya mwili kuharibika, ulizikwa siku hiyo hiyo majira ya saa 10 jioni.

Polisi mkoani humo ilithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba wanaendelea na uchunguzi.

Mkazi wa Mtaa wa Mchema, Ally Salvatory, alieleza kusikitishwa na tukio hilo la kikatili na kuiomba jamii kushirikiana kwa karibu. Aidha, baadhi ya wakazi waliliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina wa tukio hilo ili kukomesha matukio kama hayo.

# Shahidi wa kesi ya Ole Sabaya ageuziwa kibao

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAWAKILI wa utetezi, katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, wamewasilisha ombi mahakamani la kukamatwa kwa shahidi wa 10 wa Jamhuri, Francis Mroso, wakidai kwamba alitoa rushwa ya Sh. milioni 90.

Akiwasilisha mahakamani ombi hilo mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Wakili wa Utetezi, Fridolin Bwemelo, alidai Sheria ya Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(IB), inaeleza wazi hatua za kuchukuliwa kwa mtu atakayetoa na kupokea rushwa na hakuna kifungu kinachoeleza kuna rushwa ya kulazimishwa.

Alidai kwa mujibu wa kifungu hicho, hakuna sehemu imezungumzia suala la kutoa rushwa kwa kulazimishwa kwa kuwa mtoaji na mpokeaji wa rushwa watakuwa wametenda kosa.

"Mheshimiwa Hakimu, tunajiuliza ni kwa nini mtu aliyetoa rushwa na kukiri mbele ya mahakama hii bado yuko huru wakati waliopokea rushwa wameshtakiwa na wako ndani. Maombi yetu ili kuondoa utata kwenye jamii inayotuzunguka, tunaomba shahidi huyu akamatwe," alidai Wakili Bwemelo.

Wakili huyo alidai kwamba mahakama imejiridhisha kupitia kwa shahidi ambaye yuko chini ya kiapo na kukiri kwamba alitoa rushwa ya Sh. milioni 90 na kwamba kesi hiyo ilipaswa kusikilizwa na mawakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na si mawakili wa Jamhuri kama ilivyofanyika katika shtaka hilo.

Baada ya hoja hizo, mawakili wa serikali, Felix Kwetukia na Tersila Gervas, walidai kwamba kwa kuwa wametuhumiwa kwamba hawakutakiwa kusikiliza kesi hiyo, watawasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), ili kutoa ufafanuzi kwa nini walipewa ridhaa ya kusimamia kesi hiyo badala ya TAKUKURU. "Tunaomba wiki mbili tuwasiliane na DPP, aliyetutuma kufanya kazi hii kwa sababu hata sisi tumetuhumiwa pia," alidai Gervas.

Baada ya ombi hilo, hakimu aliahirisha shauri hilo hadi leo atakapotoa uamuzi mdogo endapo ombi la kukamatwa kwa shahidi huyo kama lina mashiko.

Katika hatua nyingine, mahakama hiyo imetupilia mbali pingamizi la mawakili wa Jamuhuri wakitaka maelezo ya Mroso aliyoandika kituo cha polisi yasipokelewe mahakamani kama kielelezo cha ushahidi kwa kuwa utaratibu wa kisheria haukufuatwa.

Pingamizi hilo, liliwasilishwa mahakamani na Kwetukia na Gervas, mbele ya Hakimu Kisinda kwamba Mroso ambaye ni mfanyabiashara katika Jiji la Arusha, alikamilisha kutoa ushahidi wake mahakamani huko. Akitoa uamuzi mdogo jana, Hakimu Kisinda, alitupa ombi la upande la mashtaka kwa kuwa haliendani na matakwa ya kifungu cha sheria ya ushahidi.

Awali Wakili Fridolin Bwemelo, aliwasilisha ombi la maelezo aliyoandika shahidi kituo cha polisi na nyaraka kupokewa kama kielelezo cha ushahidi mahakamani.

Bwemelo, alidai kwamba maelezo yaliyoandikwa na shahidi huyo yanatofautiana na ushahidi wake alioutoa mahakamani.

# TMA yaonya mvua kubwa inakuja

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeshauri wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayoathiriwa na mafuriko katika mikoa kadhaa kuchukua hatua kwa kuwa mvua za msimu kubwa zimeanza.

Mikoa hiyo ni ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba na kwamba kunategemewa kuwa na vipindi vya mvua kubwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya TMA iliyotolewa jana mchana, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi huu.

Aidha, mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika maeneo mengi ya nchi, hivyo kuondoa ukame kwenye baadhi ya maeneo ya nchi.

"Kwa upande wa Nyanda za Juu Kaskazini kwa maana ya mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara, tunatarajia kuwapo kwa vipindi vichache vya mvua katika maeneo machache, lakini kwa wiki ijayo tunatarajia ongezeko kidogo la mvua kwa mikoa hii," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Hata hivyo, ilisema kwa upande wa Kanda ya Ziwa mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu licha ya vipindi vya mvua kuendelea katika baadhi ya maeneo, upungufu wa mvua unatarajiwa kutokea katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi huu.

"Kwa mikoa ya magharibi ya nchi yetu kwa maana ya mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora vipindi vya mvua vinatarajiwa kwa mikao hiyo, lakini tunatarajia ongezeko kidogo katika wiki ya nne ya mwezi huu. Hali hiyo pia inatarajiwa kwenye mikoa ya Kanda ya Kati kwa maana ya Singida na Dodoma na Nyanda za Juu Kusini Magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro," ilieleza.

Pia kwa mikoa ya Lindi na Mtwara kunatarajiwa kuwapo kwa mvua za kawaida na ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya tatu ya mwezi huu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa TMA, Mkoa wa Ruvuma unatarajiwa kuwa na upungufu wa mvua wiki ya tatu ya mwezi huu.

Kwa mwezi Januari, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo, hata hivyo hali ya joto inatarajiwa kuwa ya kawaida.

# Komandoo mwingine adai kuteswa polisi

**Na Kulwa Mzee**

KOMANDOO Gabriel Mhina amedai alikamatwa mkoani Tabora, alisulubiwa na kupigwa kwa saa tatu na askari polisi, akitakiwa kueleza uhusiano alionao na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe.

Amedai kuwa baada ya kukataa kuwa na uhusiano na kiongozi huyo, aliteswa zaidi.

Shahidi huyo wa tatu upande wa utetezi alikuwa mshtakiwa kwenye kesi ya ugaidi, akaachiwa baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati ya kuwaondoa kwenye kesi pamoja na wenzake wawili Julai 27, mwaka huu.

Amiri alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati akitoa ushahidi upande wa utetezi kwenye kesi ndogo ndani ya kesi kubwa ya ugaidi.

Akiongozwa na Wakili Dickson Matata, alidai Septemba 19, mwaka 2020, alipigiwa simu na rafiki yake anayeitwa Dida wakaangalie mpira Oxygen Pub, maeneo ya Makokora mkoani Tabora.

Shahidi huyo alidai akiwa eneo hilo, ghafla alikamatwa na askari wa kikosi maalum, mmoja akimtolea bastola na kumfahamisha anahitajika kwa RCO.

"Nilikubali kupanda gari lao, Toyota Land Cruiser jeusi, kwenye gari nilikuwa mimi na wao watatu, nilikaa mbele na dereva hadi Kituo cha Polisi Tabora.

"Wakati ninasubiri kuonana na RCO walinifunga pingu wakanipeleka ndani ya kituo nyuma, waliniuliza 'kesho kuna tukio gani?' Nikasema kuna ujio wa Rais Magufuli, anakuja kufanya kampeni.

"Kule nyuma walinihoji nina uhusiano gani na Mheshimiwa Mbowe huku wakinipiga vibaya kila sehemu ya mwili wangu, walinipiga kwa kutumia fimbo, ngumi kwenye taya na mateke.

"Alikuwa Goodluck, kiongozi wao alikuwa afande Jumanne, kulikuwa na Minja na afande Aziz, mmoja simkumbuki.

"Nilipigwa kwa saa tatu, nilipokuwa nakataa kuwa na uhusiano na Mbowe walinipiga zaidi, wakanipeleka Kituo cha Polisi cha Reli Tabora maana hali yangu ilikuwa mbaya," alidai Mhina.

Alidai kuwa wote waliokuwa wanamsulubu ndio waliompeleka Kituo cha Reli na kumfuata siku iliyofuata Septemba 20, 2020 saa nne asubuhi. Shahidi alidai walimuuliza kuhusu mshtakiwa wa tatu Mohammed Ling'wenya kama anamfahamu, alikiri anamfahamu na aliwahi kufanya kazi naye Kikosi cha Makomandoo 92 KJ Ngerengere na alipotoka kazini alikuwa rafiki yake wa karibu.

Alidai kuwa asubuhi saa tano, alipelekwa Nzega akiwa amefungwa pingu na kafungwa kitambaa usoni, walipomfikisha Kituo cha Polisi Nzega walimwacha na hakujua walikokwenda.

"Walirudi siku ya pili wakiwa na Malema ambaye alishawahi kuwa komandoo. Nilimfahamu komandoo kwa sababu mazingira yake ya kukamatwa yalikuwa kama yangu.

"Nilimuuliza alisema alikuwa komandoo, siku inayofuata tulianza safari ya kupelekwa Dar es Salaam, kila mtu na gari lake," alidai Mhina.

Alidai kuwa walipotoka Nzega, walifikishwa Kituo cha Polisi Tazara, mahabusu na askari walimfahamisha palikuwa Tazara.

Shahidi huyo alidai alifika Tazara Septemba 23, 2020, akakaa siku mbili na ilipofika Septemba 25 alifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa tuhuma za ugaidi.

Alidai kuwa akiwa Tazara, mahojiano yalikuwa yakifanyika juu kulikokuwa na chumba, alidai Malema alihojiwa na Inspekta Mahita Omari na yeye alihojiwa na SP Jumanne.

Shahidi huyo alidai aliambiwa ataunganishwa na wenzake kwenye kesi ya ugaidi namba 63/2020 na kwamba akiwa Tazara, alikuwa anakunywa maji tu, chakula alikula Septemba 25 gerezani baada ya kutoka mahakamani.

"Julai 27, mwaka huu, tulipofika mahakamani, Hakimu Thomas Simba alisema serikali haina nia ya kuendelea na shauri letu, nikaachiwa mimi, Kaaya na Khalid.

"Tukiwa gerezani Ling'wenya alinifahamisha mateso yote aliyokuwa akiyapata tangu Moshi alipokamatwa hadi Dar es Salaam," alidai Mhina.


EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI HUDUMA NA KUFUNGA (PAMOJA NA UTOAJI WA MAFUNZO KWA MTUMIAJI) MTANDAO WA KUTOA TAARIFA.**
**KUMBUKUMBU: 0010007310**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inahitaji huduma za kampuni au shirika lililo na uzoefu uliothibitishwa wa kuunda,kusakinisha,na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mwisho kwa huduma inayofuata ya dawati la usaidizi na kwa mfumo wa kuripoti maudhui ya ndani ya mtandao (LCRP) kwa ajili ya mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unahitaji watoa huduma wenye uzoefu na uwezo yakinifu wa kutoa huduma za kutengeneza na kusimika mfumo wa Mtandao wa kutoa taarifa (LCRP) unaokidhi hitaji na vigezo vifuatavyo:

- Mfumo unaohifadhi taarifa katika mtandao na unaoweza kuzuia ufikikaji katika baadhi ya vipengele kwa watoa huduma na mashirika kwa kuwa na nenosiri litakalo tolewa na Mradi wa EACOP Pamoja na nenosiri linaloweza kudhibitiwa..
- Inayoruhusu usajili wa watoa huduma wa nchini Uganda na Tanzania kuweza kupata taarifa kuhusu taarifa ya ombi la Kuonesha Nia (EOI).
- Inayowezesha wasambazaji kutoa ripoti ya mafanikio na maendeleo ya Watoa huduma wa ndani katika fomu zinazolindwa na nenosiri na zinazo iwezesha EACOP kutizama mwendendo wa wasambazaji kwa kulinganisha na taarifa za siku ya kikomo.
- Uwezo wa kuchanganua data ya maudhui ya muuzaji ,msambazaji, wa ndani na kuandaa ripoti kwa kuzingatia matakwa ya mamlaka yan chi za Tanzania na Uganda na kuchambua mwenendo kwa kulinganisha na matarajio.
- Watoa huduma wanahimizwa kuelezea uwezo wowote wa ziada wa utendaji uliopo au unaowezekana kuwa na manufaa kwa EACOP, na uwezo wake wa kujenga uwezo kwa watoa huduma .
- Uwasilishaji wa ana kwa ana au kwa kutumia Programu kwa watumiaji na watoa huduma kwa kutumia lugha zaidi ya moja.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yanayoonyesha nia yao yanahitajika kuwasilisha taarifa zifuatazo:

- Rekodi ya kina ya utendakazi, na uwezo wa kutengeneza na kusimika programu ya computer inayoweza kukidhi hitaji na inayotuza taarifa katika mtandai, kufundisha watumiaji na kuwa na lugha zaidi ya moja (hususani Kiswahili na Kiingereza), dawati la usaidizi kwa Tanzania na Uganda, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Wafanyakazi wanaokidhi na wenye uzoefu wa kuweza kuelewa mahitaji ya Mradi wa EACOP kwa kuzingatia sheria za Watoa Huduma wa nchini Tanzania na Uganda na kutengeneza programu ya kompyuta.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia au
  Uthibitisho wa usajili katika Kanzi Data ya watoa Huduma wa ndani nchini Uganda wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za nchini Tanzania/Uganda pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, usalama na Mazingira, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa leseni ya usajili kutoka kwa mamaka husika nchini Tanzania/Uganda kwa ajili ya utoaji wa huduma tajwa.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** Jioni Afrika Mashariki (EAT) tarehe **23rd, December 2021.** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007310**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa

HABARI KITAIFA

# Tanzania yanadi vivutio utalii kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,** MADRID

TANZANIA inashiriki Mkutano Mkuu wa 24 wa Kimataifa wa Utalii Duniani ulioanza jana jijini hapa huku ikitumia jukwaa hilo kwa ajili ya kunadi vivutio vya utalii vilivyoko nchini.

Katika mkutano huo wa siku ulioandaliwa na Shirika la Kimataifa Utalii Duniani (UNWTO), Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ameweka bayana mambo mbalimbali ambayo Tanzania itanufaika na mkutano huo.

"Katika kuhakikisha tunaongeza idadi ya watalii kuitembelea Tanzania na mapato yatokanayo na utalii, suala la kutangaza utalii wa Tanzania katika nyanja za kidunia ni suala ambalo haliepukiki," alisema.

Alitaja moja ya maeneo ya kutangaza utalii huo ni kuhudhuria mikutano mikubwa duniani ambayo inahusisha masuala ya utalii ikiwamo kuja nchini Hispania ambako ndiko yaliko makao makuu ya utalii duniani katika jiji la Madrid.

Katika siku ya kwanza ya mkutano huo, Tanzania ilipata fursa kadhaa ikiwamo kutumia mkutano huo kutangaza vivutio vilivyoko Tanzania, kuiambia dunia nzima kwamba Tanzania iko salama na kuwataka watalii kuja kujionea vivutio vya utalii ilivyo navyo.

"Watalii waje Tanzania wauone Mlima Kilimanjaro, waje Tanzania waione Serengeti, waje Tanzania waione Ngorongoro na waje Tanzania waone fukwe nzuri zenye mchanga mweupe Zanzibar. Waje Tanzania waone vivutio mbalimbali ambavyo tuko navyo," alisema Dk. Ndumbaro.

Dk. Ndumbaro aliongeza kuwa katika mkutano huo, Tanzania itatia saini mkataba na UNWTO wa kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 65 wa Utalii Barani Afrika ambao utafanyika Oktoba 6 hadi 8, 2022 jijini Arusha.

"Mkutano huu tunauleta kwa sababu ni fursa nyingine kwa Tanzania. Tulishapewa nafasi kuwa mwenyeji wa mkutano wa utalii wa Kanda ya Afrika kule nchini Cape Verde, lakini sasa tumekuja kutia saini makubaliano ya kuwa wenyeji wa mkutano huo. Baada ya kutia saini sasa tutakuwa na uhakika asilimia 100 na tumetengeneza 'Post card' ambapo kila mshiriki aliyekuja hapa tunampa kusaidia sana kutangaza utalii wa Tanzania," alisema.

Pia alisema suala la tatu kwenye mkutano huo, Tanzania imekuwa katika mstari wa mbele kupigania haki za watalii na itashiriki kuhakikisha sheria ya kimataifa inapitishwa.

"Jambo lingine ambalo tunalifanya katika mkutano huu ni kupitisha sheria ya kutetea haki za watalii duniani pale inapotokea matatizo. Tumejifunza kutokana na kadhia ya janga la corona kwamba nchi zilifunga mipaka na baada ya nchi kufunga mipaka, watalii walikuwapo kwenye nchi zingine na hawaweza kurudi.

"Sasa haki zao zilikuwa hazijawezi kutetewa na sheria za kimataifa. Kwa hiyo sasa tunapitisha sheria ya kimataifa ya kutetea watalii katika mazingira ya dharura kama hayo. Ni sheria ambayo itaongeza heshima ya biashara ya utalii duniani kwa sababu unapolinda haki ya mtalii, mtalii anajiona yuko salama zaidi kuja na kushiriki katika nchi yako. Tanzania tumekuwa mstari wa mbele kuhakikisha sheria hiyo inapita," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema mkutano huo una faida nyingi kwa Tanzania katika kuhakikisha inatimiza idadi ya watalii milioni tano na mapato zaidi ya Sh. bilioni sita.

"Tunatumia mkutano huu kama fursa ya sisi kutangaza utalii, lakini kama fursa ya kuwavuta wenzetu waje pia. Tumepongezwa kwa namna ambavyo tumeweza kufanya onyesho la kwanza la utalii katika nchi za Afrika Mashariki.

"Sisi tuliona dogo, lakini wenzetu huku katika nyanja za kimataifa tumepongezwa na nimesema kwamba kumbe kweli Watanzania wanaweza kufanya mikutano kwa kiwango kikubwa zaidi," alisema.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akikata utepe kuzindua mnara wa simu wa 4G kwa wananchi wa Kijiji cha Matuli, Kata ya Matuli, Wilaya ya Morogoro, baada ya serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na Kampuni ya Simu ya Airtel, kujenga mnara huo, ili kuwawezesha kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Wengine ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela (mwenye miwani) na (kushoto) ni Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Hamisi Shabani 'Babu Tale'. Habari Uk. 10. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi afunguka msako mauaji ya dada wa Msuya

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa pili, Mrakibu wa Polisi, (SP) David Mhanaya (54) katika kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi inayomkabili mke wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita na mwenzake, amedai mahakamani kwamba aliagizwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Diwani Athumani, kuongeza nguvu ya upelelezi wa mauaji ya Aneth Msuya.

Alidai kuwa, Agosti 4, 2016 akiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, bosi wake Diwani (kwa sasa Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa) alimpa maagizo ya kuungana na askari wengine kwenda Mkoa wa Kipolisi Temeke kuongeza nguvu kwenye upelelezi wa kesi ya mauaji hayo.

Ushahidi huo, aliutoa jana katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Jaji Edwin Kakolaki. Shahidi alidai kuwa baada ya kufika Temeke, akiwa na wenzake aliripoti kwa Mkuu wa Upelelezi (RCO), Mrakibu Mwandamizi, (SSP) Mchomvu baada ya kubadilishana taarifa za kipelelezi, walijulishwa kwamba mhusika wa mauaji yuko Arusha.

"Tuliamriwa mimi, Mrakibu Msaidizi (ASP), Jumanne Malangai, Inspekta Latifa Chico na dereva Konstebo Yahaya kwenda Arusha kwa ajili ya kumkamata na kumfikisha Temeke mtuhumiwa," alidai shahidi.

Alidai kuwa walianza safari siku hiyo saa 5:00 usiku na walifika Agosti 5, 2016 wakaripoti kwa RCO Arusha, SSP George Katabazi saa 3:00 asubuhi.

"Tuliwasiliana na infoma muda wote wa mchana, saa 11:45 alasiri alitujulisha kwamba mtuhumiwa yuko Tembo Club, tulikwenda njia ya kwenda Monduli, kweli alikuwapo anakula, tulisubiri amalize nikamwagiza Inspekta Latifa kwenda kumkamata, alijitambulisha na alimkata," alidai SP Mhanaya. Alidai kuwa baada ya kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa walifuata taratibu zao kwenda kumfanyia upekuzi nyumbani kwake na baadaye waliagana na mwenyeji wao RCO Arusha wakarejea jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa walifika Temeke saa 3:00 usiku alimwagiza Inspekta Latifa kumkabidhi mtuhumiwa kwa kiongozi wa ulinzi wa kituo kwa ajili ya kumweka mahabusu.

Alidai kuwa DCI alikuwa akiwasiliana na RCO wa Arusha na wa Temeke kama taratibu zao zinavyoelekeza.mbali na Mrita, mshtakiwa mwingine ni, Revocatus Muyella. Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na shtaka la kumuua kwa makusudi Aneth Msuya, dada wa marehemu bilionea Erasto Msuya Mei 25, 2016, eneo la Kibada Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

## TMDA yakiri udhibiti dawa bandia ni tatizo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Nyanda za Juu Kusini, imesema zaidi ya asilimia 80 ya dawa zinatoka nje hivyo ni changamoto licha ya kwamba udhibiti wake umeimarishwa mipakani.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa TMDA, ni kutokana na uwapo wa dawa duni na bandia ambazo hazijasajiliwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Kaimu Meneja wa TMDA Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wakaguzi wa dawa ngazi ya halmashauri mkoani Njombe. Alisema uwapo wa dawa hizo hauna budi kufuatilia na kuondolewa katika soko.

"Mamlaka inahitaji wakaguzi wenye weledi katika kutambua dawa, vifaa tiba na vitenganishi visivyofaa kwa matumizi pamoja na kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji na ukuaji wa viwanda vya dawa, vifaa tiba na vitenganishi hapa nchini ili kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje," alisema.

Pia alisema katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuna matukio ya ukiukwaji wa sheria ya dawa na vifaa tiba kutokana na watu kuuza dawa ambazo hazijasajiliwa kwa maana hazitambuliki ubora na usalama wake.

"Dawa aina hizo mara nyingi zinaingizwa kinyemela sasa. Unajua ukanda wetu huu tuna mipaka ya karibu ambapo dawa ambazo hazitambuliki zinaingia nchini kinyemela. Pia kuna changamoto ya watu kuuza dawa ambazo zimeghushiwa zimeisha muda wa matumizi lakini anabadilisha, anauza hivyo hivyo," alisema Mshighati.

Mgeni rasmi katika mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Dk. James Ligwa, aliwataka wataalamu kuhakikisha wanachukua hatua stahiki kwa wafanyabiashara wanaokiuka sheria na taratibu za biashara ya dawa na vifaa tiba kwa kuwa wanapoachwa, wanahatarisha afya za Watanzania.

"Pia nawahimiza TMDA kwa kushirikiana na halmashauri endeleeni kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili watambue kwa urahisi bidhaa zisizofaa. Wafanyabiashara nao wapewe elimu ili kutii sheria bila ya shuruti," alisema Ligwa.

Naye Mfamasia wa Mkoa wa Njombe, Juma Mang'ombe, alisema mkoa kwa kushirikiana na mamlaka, umedhibiti kusambazwa kwa bidhaa ambazo ziko chini ya kiwango pale zinapokuwa zimegundulika.

HABARI KITAIFA

# Waziri apata mbinu kundi maalumu kutoa Rais nchini

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga, amelitaka kundi la watu wenye ulemavu lijiamini linaweza na kuchangamkia fursa zikiwamo za elimu ili siku moja litoe rais wa nchi.

Nderiananga aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kongamano la kitaifa la kuzungumzia ukatili wa kijinsia dhidi ya watu wenye ulemavu ambalo limekutanisha watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wadau wa maendeleo na wahusika.

Kongamano hilo lilikwenda sambamba na uzinduzi wa mradi mpya wa dola za Marekani milioni sita wa Shirika la Idadi ya Watu Ulimwenguni (UNFPA) uitwao 'Chaguo Langu, Haki yangu,' ambao umefadhiliwa na Serikali ya Finland na unatekelezwa na Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF).

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Nderiananga alisema Rais Samia Suluhu Hassan, analipenda kundi hilo ndiyo maana ametoa Sh. bilioni nane kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vinne vya watu wenye ulemavu na kuvikarabati vilivyopo.

"Tutajenga chuo kipya cha kisasa Kasulu, Kigoma na Songwe, Mbozi, upo mchakato unaoendelea ofisini kwangu, tutajenga chuo kimoja Shinyanga kwa fedha za mdau wa maendeleo ambaye amejitolea kutusaidia," alisema.

Aliongeza kuwa uwapo wa vyuo hivyo ukiunganisha na miradi mbalimbali, utasaidia kutoa elimu na kundi hilo lifanye vizuri.

Alisema kwa pamoja wakichukua hatua za kupinga ukatili dhidi ya kundi hilo, itasaidia kujenga jamii yenye mshikamano na inayoheshimu usawa na haki za binadamu.

Nderiananga alisema fedha za mikopo zinazotolewa na halmashauri mbalimbali zinaonyesha wanaorejesha vizuri ni watu wenye ulemavu na kuwataka wazichangamkie ili kukuza vipato vyao.

Pia aliwataka katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwakani, wasijifungie ndani wajitokeze ili kuiwezesha serikali kujua idadi yao na kuweza kupanga vizuri mipango yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema maeneo ambayo mwaka huu wamechagua ni kundi hilo na kwamba matatizo yatakayoibuliwa kwenye mdahalo huo yatawasilishwa serikalini kwa hatua zaidi.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA nchini, Jacqueline Mahon, alisema mradi huo ni wa miaka mitatu na nusu wa kuwafikia wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili wachukue hatua za maisha yao na kufurahia haki zao.

Alisema takwimu za sensa ya mwaka 2012 zinakadiria kuwa asilimia 9.3 ya watu wa Tanzania wanaishi na ulemavu ingawa hazijajumuisha vijana au watoto kwenye kundi hilo.

Balozi wa Finland nchini Tanzania, Ritta Swan, alisema mradi huo unagharimu dola milioni sita.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Hamad Masoud Hamad (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu nia yake ya kutaka kugombea nafasi ya uenyekiti taifa wa chama hicho, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Januari 29 mwaka kesho. Kulia ni Mshauri wa Amani wa chama hicho, Hamad Mmanga Khalfan. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kigogo ACT atangaza nia ya kumrithi Maalim Seif

**Na Christina Mwakangale**

KADA wa Chama cha ACT-Wazalendo, Hamad Masoud Hamad, ametangaza nia ya kugombea uenyekiti wa taifa wa chama hicho kumrithi Hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

Amesema anao uwezo wa kuvaa viatu vya Maalim Seif kutokana na alivyomjenga kuwa kiongozi tangu akiwa kijana.

Amesema amefanya kazi na Maalim Seif tangu mwaka 1992, akiwa kijana pekee kwenye siasa kipindi hicho, hivyo uzoefu alionao unatosha kushika nafasi anayoiwania.

Masoud, ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Miundombinu Zanzibar, kabla ya kujiuzulu kutokana na ajali ya meli ya Mv Islanders, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kusudi la ACT-Wazalendo, kuitisha mkutano mkuu wa taifa wa dharura Januari 23, mwakani.

Alisema mkutano huo umelenga, kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Maalim Seif pamoja na iliyo wazi baada ya kujiuzulu kwa Makamu Mwenyekiti, Juma Duni Haji.

"Ninaweza kuvaa viatu vya Maalim Seif, bila kuchechemea. Maalim ameniacha vizuri. Tofauti ya Maalim na mimi, ni jina, umri, ila nina uwezo wa kuongoza, ninafanana naye kwa hoja naamini katika maridhiano," alisema Masoud.

"Nimefanya kazi na Maalim takribani miaka 30, nilikuwa karibu nae tangu kuanzishwa kwa CUF, na ni kijana pekee niliyejitoa kufanya kazi na wazee hawa ambao wote walikuwa wakubwa kwangu."

"Siasa si nguvu ya ushindani, nikipata ridhaa, nitazingatia kutatua kero za wananchi, kujenga mtandao wa chama na kilicho makini, nitaanzisha dawati maalum kusikiliza kero, kuondoa sheria kandamizi na kufanyia marekebisho."

Alisema, atasimamia na kudumisha serikali ya umoja wa kitaifa na kwamba atahakikisha Zanzibar inakuwa mamlaka kamili, na kwamba atahakikisha chama chake kinajizatiti katika ngazi ya majimbo, mikoa na taifa na kubuni njia ya kujipatia mapato ili kujiendesha.

"Tutashirikiana na vyama vingine, taasisi mbalimbali na wadau kuleta msukumo kuhakikisha upatikanaji wa katiba mpya, na tume huru ya uchaguzi. Chama kitajizatiti kuhakikisha hakiporwi ushindi wake kwenye uchaguzi mkuu na serikali za mitaa, ujao," alisema Masoud.

**SHELL TANZANIA LIMITED**
Cheti cha usajili namba 16839
*Sheria ya Makampuni, 2002*
(KIFUNGU 334 (1))

**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha **Shell Tanzania Limited** (kampuni), yenye usajili namba 16839, Kwenye kikao kilichofanyika tarehe 1 November 2021 azimio maalumu lilipitishwa:

1. kufuatana na kifungu 333 (1)(b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ivunjwe kwa hiari; na
2. Wanahisa wamemteua Joseph Lyimo wa Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelatini (30). Madai yote yafungwe ndani ya bahasha na yatumwe kwa JOSEPH LYIMO wa PricewaterhouseCoopers ya Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania, ambaye ni mfilisi wa kampuni. Maombi yote yatakayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

Imetolewa na:

**JOSEPH LYIMO**
MFILISI wa SHELL TANZANIA LIMITED

**Tafadhali zingatia hii ni kampuni ya zamani ya shell ambayo ilikuwa inajishughulisha na biashara ya usambazaji wa mafuta (downsteam) na sio Shell Exploration and Production Tanzania Limited-TZ Branch ambayo inajishughulisha na biashara ya uchunguzi na uchimbaji wa mafuta na gesi (upstream).**

216596602

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Katazo la waziri masomo wakati wa likizo ni sahihi

**JANUARI** na Septemba mwaka huu, gazeti hili liliandika habari za kina zikieleza ni kwa jinsi gani wanafunzi wanabeba mabegi mazito ambayo ni hatari kwa afya zao, huku muda wa kusoma ukiongezwa kuliko ratiba iliyowekwa na serikali.

Hali hiyo imeonekana zaidi kwa shule binafsi ambazo wanafunzi wa madarasa ya mitihani yaani la nne na la saba wanabeba mabegi yenye madaftari mengi kwa kuwa wanatakiwa kubeba na madaftari ya nyuma, hali ambayo imesababisha matatizo ya kiafya kwa baadhi ya watoto ambao wazazi wao walizungumza na gazeti hili.

Aidha, baadhi ya shule muda wa likizo uliowekwa na serikali hutumika pia kwa wanafunzi kwenda shuleni huku wakibaki shule hadi usiku pale wenzao wanapoondoka, na kwa wanaolala shuleni husoma hadi usiku jambo ambalo linaathiri kisaikolojia.

Lengo la kuibuliwa kwa habari hizi ni kuonyesha tatizo lilipo, ukubwa wake na namna litasababisha madhara makubwa kwa wanafunzi ambao ni taifa la kesho, na sasa serikali na wadau wengine wamesikia na kutangaza kuchukua hatua madhubuti.

Baada ya kuandikwa kwa habari hizo, wiki iliyopita Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), kilitangaza kufanya utafiti wa kiafya kwa wanafunzi kuwekwa shuleni kwa muda wa ziada, pia kulazimishwa kubeba mzigo mkubwa wa vitabu.

Juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alitangaza kupiga marufuku masomo ya ziada shuleni, muda wa masomo wakati wa likizo kwa kuwa wanatakiwa kupumzika na siyo kuendelea na masomo.

Alisema walichobaini wanafunzi hawapumziki kutokana na baadhi ya shule za msingi na sekondari kulazimisha muda wa ziada, na kutaka muda wa masomo uheshimiwe kwa kuwa watoto wakifunga shule wanatakiwa waende nyumbani na kama kuna ulazima wa masomo ya ziada lazima kuwe na kibali kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

Waziri Ummy alibainisha kuwa kuna siku 194 za masomo zina miongozo ambayo ikitumiwa vizuri inatosha kusoma.

Tunawapongeza MAT kwa kusikia kilio hicho, sasa wameanzisha utafiti ambao utasaidia kuonyesha matokeo ya kisayansi ili kuthibitisha athari zilizoelezwa kwa wanafunzi hao, jambo ambalo litakwenda kubadilisha utaratibu kwenye shule hizo kuwa na makabati au droo za wanafunzi kuhifadhia mali zao.

Shule za kimataifa au katika nchi zilizoendelea kila mwanafunzi anakuwa na kabati au droo lake la kuhifadhia mali zake na huenda nyumbani na zile atakazotumia kwa siku hiyo na hata akifika shuleni huingia darasani na daftari atakalotumia.

Kwa nchini kwetu wanafunzi wanabeba mzigo mzito jambo ambalo ni hatari kwa afya zao, na ukifuatilia kwa kina ni kwa kuwa shule zinakwepa gharama ya kuwa na droo ya kila mwanafunzi kuhifadhi mali zake na kuwa na ufunguo wake.


Tunaipongeza serikali kwa kuingilia kati kwa kupiga marufuku, lakini tunaishauri ifuatilie kwa karibu ili kuwa na utekelezaji vinginevyo itabaki kuwa ni maelekezo ambayo bado wahusika hawatekelezi.

Serikali iliwahi kutaka wamiliki wa shule kuhakikisha mabasi yanayobeba wanafunzi ni yenye rangi ya njano, lakini hadi sasa kuna shule zinatumia magari ya kawaida na wengine daladala zinazotumika kwa usafiri wa umma.

Kukiwa na ufuatiliaji wa karibu kutaisaidia kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwa muda unaotakiwa kisheria, pia shule zinakuwa na droo au kabati kwa kila darasa kuhifadhi mali zao ili kuachana na tabia ya kuwabebesha mizigo wanafunzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Ukimwi bado upo, kila mmoja akubali kumkinga mwingine

**"NAWASISITIZA** vijana, Ukimwi bado upo, lazima kila mmoja akubali kumkinga mwingine, hii itatusaidia kuokoa nguvukazi ya taifa na kuipa nafuu serikali katika kugharamia masuala ya Ukimwi".

Ni kauli ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alipozungumzia kwenye kilele cha Siku ya Ukimwi Duniani.

Shughuli hiyo ilianza Novemba 24 na kufika kilele chake jana, huku kitaifa ilifanyika jijini Mbeya ikiendana na kaulimbiu "Zingatia Usawa. Tokomeza UKIMWI. Tokomeza Magonjwa ya Mlipuko."

Waziri anasema, licha ya kuwapo na mafanikio katika mapambano dhidi ya Ukimwi, bado kuna maeneo yanayohitajika nguvu zaidi, ili kutokomeza VVU na Ukimwi ifikapo mwaka 2030.

Maana yake nini? Anataka baadhi ya maeneo ambayo yanatakiwa kuwekewa mkazo zaidi kuwa ni kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi na VVU, hasa kwa vijana, kwa kuwa zaidi ya theluthi moja ya maambukizi mapya hutokea kwa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24, hususan wa kike ambao ni robo tatu ya waathirika.

Hapo kuna maana, vijana wanatakiwa kuelekezwa namna ya kujikinga na maambukizi mapya, hali kadhalika wakubali kujikinga, hatua ikakayosaidia kupunguza usambazaji virusi. Ni ishara bora ya unafuu kwa vijana wengine.

Binafsi ninaamini kwamba, hatua hizo zilizotangazwa na serikali kuendelea kupambana na maambukizi mapya ya VVU na Ukimwi zitasaidia kuifanya jamii kuwa salama na kuendelea kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

Pamoja hayo, hatua hizo pia zitasaidia kuokoa vijana ambao ndiyo nguvukazi na taifa la kesho, ili wawe makini katika kulinda afya zao kwa kuepuka vishawishi vyote vinavyoweza kusababisha wapate ugonjwa huo. Waziri anasema, serikali imepiga hatua kudhibiti maambukizi ya VVU na Ukimwi kwamba upimaji wa hiari wa maambukizi ya virusi vya Ukimwi umeongezeka kutoka asilimia 61 mwaka 2016 hadi asilimia 83 mwaka 2019.

Ni vyema mwamko huo wa upimaji kwa hiari, ukaendelea kuongezeka katika jamii, ili kila Mtanzania ajue hali yake kwa ajili ya kupunguza pia kiwango cha maambukizi mapya katika jamii. Msisitizo wa waziri kwa vijana unaeleza wao ndiyo wako kwenye hatari zaidi, na kwamba Ukimwi bado upo, ikibeba maana ni lazima kila mmoja akubali kumkinga mwingine ili kusaidia kuokoa nguvukazi hiyo ya taifa.

Muhimu si kuokoa nguvukazi ya taifa tu, pia itaipa nafuu serikali katika kugharamia masuala ya Ukimwi, kwa kuwa watakuwa wameepuka njia zote zinazochangia kuwapo kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Kimsingi, changamoto zinazowaathiri vijana zinaonekana dhahiri, ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya, ambayo huwa inaelezwa yanaweza kusababisha mhusika kupata ugonjwa wa Ukimwi.

Hiyo inatokana na uhalisia, huwa wanachangia sindano za kujidunga dawa hizo na kwamba mmoja akiwa na Ukimwi inakuwa rahisi kumwambukiza mwenzake, hivyo ni muhimu kulinda kundi hilo.

Ni muhimu vijana kufikiria kuhusu stadi zinazohitajika kwa maisha yao ya baadaye, kwa kupata taarifa sahihi kuhusu masuala mbalimbali na kujifunza stadi hizo, ili ziwasaidie kupanga maisha yajayo yenye furaha na afya njema.

Kwa ujumla, kundi hilo la vijana ndilo linaokumbwa na tatizo la mimba za utotoni, kuacha shule, kuambukizwa magonjwa ya kujamiiana maarufu kitaalamu 'STI' ikiwamo pia virusi vya Ukimwi.

Ninaamini kwamba, jamii inaweza kuwasaidia vijana hao kwa kuwapa taarifa sahihi na stadi za kuwa na mienendo bora ya afya na kubaki salama katika kipindi chote cha mabadiliko na vishawishi vya ujana.

Vijana bila Ukimwi inawezekana iwapo kila mmoja wetu atafanya sehemu yake kwa ajili kuwasaidia kukabiliana na changamoto zinazoweza kuwaingiza kwenye hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wapili kulia), akizindua Bima ya Maisha ya Mkono wa Pole kwa ajili ya wanataaluma wa fani ya Ununuzi na Ugavi (APSP), jijini Arusha jana. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Godfrey Mbanyi (kulia), Mwenyekiti wa Chama hicho, Emmanuel Chaurembo (wapili kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Ununuzi na Ugavi, Irene Isaka. Habari Uk. 10. **PICHA: MPI-**

# TANAPA yachukua hatua wanyamapori waliozama

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limekiri baadhi ya wanyamapori katika hifadhi zake kunasa kwenye matope na wengine kufa kutokana na ukame.

Baada ya kusambaa kwa video fupi ikionyesha nyati wakiwa wamenasa kwenye matope kwenye bwawa lililoko Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA) mkoani Morogoro, uongozi wa TANAPA jana ulitoa ufafanuzi kuhusu baa hilo.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa TANAPA anayeshughulikia mawasiliano, Pascal Shelutete, aliiambia Nipashe jana hali hiyo iliyosababishwa na ukame, imejitokeza kwenye hifadhi zingine zikiwamo Nyerere na Mkomazi ambako baadhi ya wanyamapori wamekufa.

"Ni kweli, tatizo la ukame limekumba maeneo ya hifadhi kama Nyerere na Mkomazi, pia baadhi ya wanyamapori wamepoteza maisha. Kwa sasa hali imeanza kurejea poa baada ya mvua kuanza kunyesha," Kamishna Shelutete alifafanua.

Katika taarifa yake aliyoitoa jana, baada ya kusambaa kwa video hiyo mtandaoni ikionyesha namna nyati wanavyojaribu kujinasua kwenye tope walikozama, Kamishna Shelutete alikiri ni ya kweli na imetokea MINAPA.

"Hali hii inatokana na matatizo ya ukame yaliyoathiri maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya hifadhi za taifa hivi sasa hasa kutokana na kuchelewa kwa mvua na hivyo kusababisha upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali ya hifadhi," alisema.

Kamishna Shelutete alisema tayari shirika limechukua hatua stahiki kukabiliana na hali hiyo ikiwamo mkakati wa dharura wa kujaza maji katika mabwawa na kuwanasua wanyamapori waliozama.

"Mikakati ya muda mrefu ni pamoja na kujenga mabwawa ya kisasa; kuondoa tope katika mabwawa pamoja na kuchimba visima virefu vitakavyotumia mfumo wa umeme wa jua," alisema.

Kamishna Shelutete alisema kwa kushirikiana na serikali za mikoa na wilaya jitihada za kuelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya maji katika vyanzo vya maji na mito zitaendelea kufanyika.

"Mvua iliyonyesha jana (juzi) jioni zimewezesha maji kiasi kujaa katika mabwawa husika na wanyamapori kurejea katika hali ya kawaida ya matumizi ya mabwawa," alisema.

Jumapili Nipashe ilimnukuu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akisema nchi inakabiliwa na ukame na tayari baadhi ya matatizo yameanza kujitokeza ikiwamo mifugo kufa, visiwa hatarini kupotea huko Pemba na mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro imekumbwa na mgawo wa maji.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) nayo ilitangaza kuwa mvua iliyoanza kunyesha ni endelevu.

Athari nyingine za ukame zilizojitokeza ni kupungua kwa kina cha maji kwenye mto Ruvu na kusababisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kutangaza ratiba ya mgawo maeneo mbalimbali.

Pia Shirika la Umeme (TANESCO) lilitangaza kupungua kwa uzalishaji wa umeme kwa megawati 345, sawa na asilimia 21, kwenye vituo vyake vitatu vya Kihansi, Kidatu na Pangani.

# Bosi TRA apongeza uadilifu wa watumishi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, amewapongeza watumishi wa mamlaka hiyo kwa kuzingatia maadili yao ya utumishi yanayohimiza weledi, uwajibikaji na uadilifu, akisisitiza ndiyo siri ya mafanikio.

Akizungumza Dar es Salaam wakati wa mapokezi ya watumishi wanamichezo wa mamlaka hiyo waliokuwa kwenye mashindano mkoani Morogoro, Kidata alisema juhudi ambazo wamezifanya watumishi hao ni kielelezo cha kuwa na nidhamu na ushirikiano siyo tu katika majukumu yao ya kikazi bali hata baina yao wenyewe.

Kamishna Kidata alisema wanamichezo hao wameibuka washindi katika michuano ya SHIMMUTA iliyofanyika Morogoro, wakitwaa vikombe vitano vya ushindi katika michezo mbalimbali.

"Ushindi huu mliouleta unaonyesha dhahiri kwamba mnazingatia maadili ya msingi yanayotuongoza ambayo ni weledi, uwajibikaji na uadilifu kwa sababu bila mambo haya matatu msingefanikiwa kuja na ushindi huu mkubwa, ninawapongeza sana.

"Napenda kuwapa taarifa nzuri wanamichezo wote kwamba, nimetoa maagizo ya kufanya matengenezo ya uwanja wetu wa mazoezi uliopo eneo la Kurasini hapa Dar es Salaam na nimetoa maelekezo kwamba ifikapo mwezi Juni, 2022 nikabidhiwe uwanja huo ili mpate uwanja mzuri wa kufanyia mazoezi," alisema.

Katika mapokezi hayo Kamishna Kidata alikuwa na mgeni wake Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato ya Uganda (URA), John Musinguzi aliyetembelea TRA kwa ajili ya kufanya mazungumzo na mwenyeji wake, Kamishna Mkuu wa TRA kuhusu masuala ya ushirikiano wa kimkakati hususani katika suala zima la ukusanyaji mapato ya serikali.

Pamoja na kuwapongeza wanamichezo hao, Kamishna Mkuu huyo wa URA alisema watafanya mazungumzo ili iandaliwe mechi ya kirafiki kati ya TRA na URA kwa lengo la kuimarisha afya ya mwili na kuongeza uhusiano mwema baina ya ofisi hizo mbili.

Mwenyekiti wa Michezo wa TRA, Zahor Salum alimshukuru Kamishna Mkuu na Menejimenti nzima ya TRA kwa kuwaruhusu, kuwaamini na kuwawezesha kushiriki michuano hiyo ya SHIMMUTA ambapo ameongeza kuwa bila kuwezeshwa na uongozi huo wasingeweza kupata ushindi huo mnono.

# Taasisi: Wadau washirikishwe waliopata mimba kurejea shule

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeshauriwa kuangalia uwezekano wa kushirikisha wadau ili kupata maoni yao katika uamuzi wa kuruhusu wanafunzi waliopata mimba kurudi shuleni.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania CEGODETA, Thomas Ngawaiya, alipokuwa anatoa maoni ya taasisi hiyo kuhusu hatua hizo zilizochukuliwa na serikali.

"Ninaamini kwamba bado nafasi ipo ya kushirikisha wadau mbalimbali katika jambo hili zito, hivyo wito wetu ni kwamba washirikishwe ili kusikia maoni yao kwamba wanasemaje," alisema Ngawaiya.

Ngawaiya aliwataja wadau hao kuwa ni viongozi wa dini, wataalamu wa elimu na watu wa kada nyingine, kwamba wanaweza kusaidia serikali kufanikisha utaratibu huo ambao tayari umeshatolewa waraka.

Alisema jambo hilo limekuwa na utata miaka mitano iliyopita tangu serikali ilipotoa msimamo wa kutoruhusu wanafunzi waliopata mimba kurudi shuleni, na kwamba, ndiyo maana wanatoa wito huo wa kushirikisha wadau.

"Sisi tunaamini kwamba, utata huo unaweza kumalizwa baada ya kushirikisha wadau na kupata maoni yao, ili kama waraka unahitaji kuboreshwa, basi wahusike kikamilifu," alisema.

Alisema, wao hawapingi wanafunzi kurudishwa shuleni, bali wanaona kwamba kuna haja ya kupata maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ili kujadili kwa kina mfumo wa kuwarejesha shuleni.

"CEGODETA tunaamini kwamba, wanaosimamishwa shule kwa sababu ya ujauzito, wanaweza kupata elimu kwa njia nyingine na ndivyo imekuwa ikifanyika miaka yote, siyo lazima warudi kwa mfumo rasmi," alisema.

Waraka huo namba Na. 2 wenye kumb.Na. ED/OK/NE/W/VOL.II/39 unaeleza kuwa pamoja na kuruhusu kundi hilo kurudi shuleni, hauwahusu wanafunzi waliofukuzwa shule kwa makosa ya jinai au mwenendo unaohatarisha amani shuleni.

Waraka huo unawashauri wanafunzi watakaothibitika kutenda makosa hayo na kufukuzwa shule, waendelee na masomo kupitia elimu nje ya mfumo rasmi.

Lakini pia unaelezea dira ya elimu ya Tanzania kuwa ni Mtanzania aliyeelimika mwenye maarifa, stadi, umahiri na mitazamo chanya ili kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Unataja lengo kuwa ni kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata fursa ya kupata elimu kama haki ya msingi bila ubaguzi wa aina yoyote, na kwamba serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza fursa na kuboresha elimu inayotolewa katika ngazi zote.

# RC ataka NHC kuwekeza maduka makubwa

**Munir Shemweta,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, amelitala Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kufikiria namna ya kuwekeza mradi wa maduka makubwa (mall) kwa lengo la kurahisisha upatikanaji huduma.

Akizungumza na uongozi wa NHC ulipomtembelea ofisini kwake juzi ukiwa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dk. Angeline Mabula, wakati wa kikao chake na Jukwaa la Wahariri Tanzania mkoani haoa, Shigela alisema kwa sasa mkoa hauna maduka kwa ajili ya kuwawezesha wakazi kupata huduma eneo moja kama ilivyo Dar es Salaam.

"Morogoro ni mji mkubwa wenye vituo vingi vyenye idadi kubwa ya watu, lakini hakuna 'supermarket' kubwa mfano wa mall, hivyo kama Shirika letu la Nyumba mfikirie namna ya kufanya uwekezaji katika eneo hilo," alisema Shigela.

Kwa mujibu wa Shigela, mbali na NHC kuwa na nyumba za makazi katika baadhi ya maeneo, uhitaji wa nyumba pamoja na maduka makubwa bado upo kwa lengo la kuwawezesha wakazi wake kupata huduma.

Alisema kwa sasa Mkoa wa Morogoro unazidi kukua kwa kasi na pia ni njia kuu ya kwenda Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Rwanda na kubainisha kuwa tayari umeanza kuainisha maeneo ya uwekezaji hasa inapopita reli ya mwendokasi.

Naibu Waziri Mabula alisema suala la kujenga 'mall' linawezekana, lakini alitahadharisha utekelezaji wake usikwamishe miradi mingine ya shirika kwa kuwa NHC imepewa ujenzi wa ofisi baadhi ya wizara katika mji wa serikali eneo la Mtumba, Dodoma

"Kujenga 'supermarket' kubwa ni jambo la kuangalia na mawazo yachukuliwe ilmradi utekelezaji wa miradi mingine isikwame. Ni lazima mjipange wajipange, wekezeni mpate pesa na biashara ni matangazo," alisema Dk. Mabula.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, aliuomba uongozi wa NHC kupitia upya gharama za kupangisha nyumba pamoja na kuzifanyia ukarabati ili ziwe na mwonekano mzuri kwa kuwa baadhi zimechakaa.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, alimhakikishia Shigela kulifanyia kazi suala hilo na kueleza kuwa shirika limekuwa na mikakati mbalimbali ikiwamo kujenga nyumba maeneo ya pembezoni.

Pia alisema katika kuhakikisha shirika linatekeleza ombi la mkuu wa mkoa wa kuangalia namna ya kufanya uwekezaji wa maduka, lilitembelea kingo za Sabasaba pamoja na Naibu Waziri kuona namna ya kufanya uwekezaji katika eneo hilo.

# Makandarasi wahimizwa kuacha kuwa waoga wanapodai haki zao

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imewataka makandarasi kuacha woga kwenye kudai haki zao pale mikataba yao inapokiukwa kwa kuhofia kuharibu uhusiano na wateja wao.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mhandisi Consolatha Ngimbwa, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kuhusu usimamizi wa mikataba kwa makandarasi wazalendo.

Aliwataka watumie ujuzi watakaoupata badala ya kuishia kwenye vitabu tu kwa kuwa uzoefu unaonyesha kwamba wako makandarasi ambao pamoja na kuwa na ujuzi, bado wanashindwa kusimamia haki zao eti kwa kuogopa kuharibu uhusiano na waajiri.

"Msifanye hivyo kwa sababu katika mikataba, mkandarasi ana wajibu na haki zake na mwajiri vivyo hivyo. Hebu jiulize kwa nini mkandarasi akikiuka makubaliano mwajiri hasiti kumchukulia hatua? Mbona mwajiri haogopi kuharibu uhusiano?" Alihoji.

Pia aliwataka makandarasi wazalendo kutokurupuka wakati wa kusoma mikataba ya ujenzi ili kuepuka hasara wanayoweza kupata na wakati mwingine kukimbia kazi wanazopewa.

Alisema usimamizi mzuri wa mikataba ni ujuzi wa muhimu na wa lazima kwa makandarasi kwa sababu kimsingi kazi ya ukandarasi ni mikataba na kwamba nyakati zote, mkandarasi anashughulika na mikataba. "Kazi yenu ni mikataba, mkandarasi atashiriki zabuni ili akifanikiwa apewe mkataba wa utekelezaji. Atatekeleza ili kutimiza makubaliano yaliyomo katika mkataba husika na mwishowe akikamilisha ataufunga mkataba husika na kadhalika. Hakuna biashara ya ukandarasi bila mkataba, hivyo hakuna mafanikio katika biashara hii bila ujuzi wa kusimamia mikataba," alisema.

Alisema kwenye mafunzo hayo watajifunza vitu muhimu katika mikataba ya ujenzi, haki na wajibu wa pande zote za mkataba, nyaraka za mikataba, hatua katika usimamizi wa mikataba, utatuzi wa migogoro, madai katika mikataba na mengineyo mengi.

Alisema lengo kubwa ni kuwajengea misingi itakayowasaidia kusimamia mikataba yenu mbalimbali vizuri zaidi.

"Nina uhakika kwamba haya yote mnayafanya katika shughuli zenu za kila siku za ukandarasi hususan mnapotekeleza miradi yenu mbalimbali. Kazi ya mafunzo haya itakuwa ni kuboresha namna ya kufanya usimamizi huo kwa kuzingatia misingi ya kitaalamu. Kupitia mafunzo haya, nina uhakika mtaongeza ujuzi wenu kwa kiwango kikubwa katika eneo la usimamizi wa mikataba," alisema.

Aliwataka makandarasi kujua umuhimu wa mafunzo ya manunuzi kwa njia ya kielektroniki (TANEPS) kwa sababu mfumo huu ndiyo njia pekee ya kuwasilisha zabuni za miradi ya serikali na kwamba serikali na taasisi zake mbalimbali ndiyo mwajiri mkubwa wa makandarasi.

Alisema CRB inazo taarifa kwamba katika TANEPS wako makandarasi ambao huwatafuta watu kutoka nje ya kampuni zao ili kuwasilisha zabuni zao katika mfumo na bahati mbaya sana ni kwamba hao watu wa nje ya kampuni wanatumiwa pia na makampuni ambayo ni washindani wao.

"Matokeo yake ni kwamba ule usiri wa zabuni yako hasa bei unakuwa haupo tena na hivyo kuwepo uwezekano mkubwa wa kukosa zabuni husika," alisema.

Msajili Msaidizi wa CRB, David Jere, aliwataka makandarasi hao kuhakikisha wanalipa ada za mwaka ili kuepuka kufutiwa usajili na kwamba kulipa ada ni wajibu wa kisheria hivyo mkandarasi asisubiri kusukumwa sukumwa kulipa.



Msajili Msaidizi wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi David Jere (kushoto), akizungumza kwenye mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa bodi hiyo, Mhandisi Consolatha Ngimbwa (wapili kushoto) na Mratibu wa Mafunzo kwenye bodi hiyo, Neema Fuime. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Chuo chajitosa ukatili watoto

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHUO Kikuu Kishiriki cha Jordan, kinachomilikiwa na Shirika la Kitawa la Wasalvatori kimeamua kusaidia watoto wanaofanyiwa ukatili.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Betram Mapunda, alisema wameamua kuanzisha kituo cha pamoja cha huduma ya mkono kwa mkono kwa ajili ya kuwasaidia waliathirika na ukatili.

Prof. Mapunda alisema zaidi ya matukio 440 yameripotiwa katika kipindi cha mwaka 2016/17 katika ofisi za kata zote zilizoko katika Manispaa ya Morogoro hatua ambayo imefanya waone umuhimu wa kuanzisha kituo hicho.

"Takribani matukio mawili mpaka nane ya kikatili yanaripotiwa kila siku na mwaka 2016/17 matukio 440 yameripotiwa katika dawati la kijinsia, hivyo ni lazima tuhakikishe tunapambana na tatizo hilo na ilijumuisha ukatili wa aina zote," alisema.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa chuo, kutokana na taarifa zilizopatikana katika warsha za viongozi na wataalamu kutoka idara ya sheria na saikolojia na unasihi walikuja na wazo la kuwa na huduma endelevu ili kuwasaidia watoto waliofanyiwa ukatili.

Naye Mratibu wa Huduma za Kituo cha Mkono kwa Mkono, Esther Andrew, alisema mradi huo umejikita kufanya kazi katika kata 15 kati ya 29 za Manispaa ya Morogoro kuwasaidia sehemu mbili zikiwamo tiba na kinga kwa watoto 700.

Kuhusu sehemu ya tiba, alisema itaunganisha tiba ya kisaikolojia inayotolewa na wamasihi na tiba ya majereha ya mwili itakayotolewa na madaktari ya magonjwa ya binadamu pamoja na tiba ya kisheria.

Alisema kwa upande wa tiba ya kinga itahusu kuelimisha jamii juu ya haki za watoto, aina na madhara ya ukatili kwa watoto na kwamba walimu waliopo katika shule hizo za kata 15 watatumika pamoja na machampioni kutoka katika kila mtaa.

HABARI KITAIFA

# SGA yashinda tuzo ya kampuni bora ulinzi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ulinzi ya SGA Security imechaguliwa kuwa kampuni bora katika kutoa huduma za ulinzi nchini Tanzania na ukanda wa Afrika Mashariki.

Hayo yamebainishwa jijini Dar es Salaam wakati wa kutoa tuzo hizo zinazojulikana kama 'Tanzania Consumer Awards 2021' iliyoenda sambamba na chakula cha jioni iliyoandaliwa na taasisi ya Lavine International Agency.

Hili lilikuwa tukio la tatu la utoaji tuzo hizo ambazo uzinduzi wake ulifanyika mwaka wa 2019 ambapo SGA Security pia ilishinda tuzo ya mtoa huduma mwenye vifaa vya uhakika katika hafla iliyofanyika mwaka wa 2020.

Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Security, Eric Sambu, alielezea furaha yake pamoja na kuridhishwa na ushindi wa tuzo hizo mbili ambazo amesema ni ishara tosha ya kuwa wateja wa SGA wana imani na kampuni hiyo ambapo amesema ushindi huo pia umetokana na wafanyakazi wa kampuni hiyo wenye weledi na uaminifu.

"Tumejitahidi sana kutoa huduma zetu kuzidi hata matarajio ya wateja wetu na tumefarijika sana kupata tuzo zinazotambua juhudi zetu haswa ikitiliwa maanani tuzo hizi zimetokana na maoni ya umma," alisema.

Alisema mafanikio hayo ya SGA ni muendelezo wa mafanikio mengine ambayo yanathibitishwa na vyeti vinne vya ISO - ISO 9001, 18788, 14001 na 45001 - ambavyo vyote vinathibitisha ubora, umakini wa SGA katika kuhudumia wateja, uwajibikaji, kuheshimu haki za binadamu na mazingira mazuri ya wafanyakazi wake katika kuhudumia wateja.

"Tuzo hizi mbili tunawatunuku wafanyakazi wetu zaidi ya 6,000 walioko maeneo mbalimbali Tanzania na zaidi ya 19,000 katika Afrika Mashariki kwa umakini wao katika kuwahudumia wateja, jambo ambalo limewajengea wao na kampuni heshima ndani ya jamii. Hawa ni mashujaa wetu na tutaendelea kuwajengea uwezo ili waweze kufanya vizuri zaidi," alisema.

Mwanzilishi wa taasisi ya Lavine International Agency, Diana Laizer, alisema tukio la utoaji tuzo hizo linalenga kutambua juhudi zinazofanywa na watoa huduma, na kwamba tuzo hizo ni motisha ili watoa huduma waendelee kuongeza juhudi.

"Upigaji kura wa mtandaoni ulifanyika kote barani Afrika ukijumuisha makundi 62 katika sekta zote za uchumi wa Afrika. Tuzo hizi zinaonyesha uaminifu wa wateja kwa watoa huduma ambao baadaye hujikita katika kutoa huduma bora", alisema.

Meneja Mauzo na Masoko wa SGA, Faustia Shoo, alisema kuwa mbali na tuzo kuonyesha imani waliyo nayo wateja kwa SGA, pia zimeonyesha wazi ya kuwa mahitaji ya soko ni huduma bora.

"Hatuuchukulii ushindi wa tuzo hizi kama kitu cha kawaida na cha kupita bali tunauchukulia kama ujumbe kutoka kwa umma unaotutaka tuongeze ufanisi katika kutoa huduma zetu katika ukanda wote wa Mashariki mwa Afrika," alisema.

# Taasisi yapania kuifanya Afrika kuwa ya kijani

**Na Christina Mwakangale**

Taasisi ya Justdiggit imelenga kuifanya Afrika kuwa ya kijani kipindi cha miaka 10 ijayo, kwa kufufua hekari 60,000 ya ardhi kavu na kupanda zaidi ya miti milioni 6.3.

Pia, imemtangaza msanii wa Bongo fleva Ben Pol kuwa balozi wa asasi hiyo na msemaji wa ndani ya bara la Afrika, kwa kushirikiana na LEAD Foundation, kutoa elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na taasisi hiyo, matumizi ya njia asilia na mbadala yanaweza kupunguza kuongezeka kwa joto duniani kwa asilimia 37 na kuongeza uelewa kwa jamii faida za kurejesha hali ya ukijani katika mazingira kwa kupanda miti na suala la mabadiliko ya tabianchi kidunia.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Justdiggit inaendesha miradi ya uwekaji na utunzaji mazingira kwa kupanda miti kwa kushirikiana na wabia, wakulima na jamii.

"Ben anajivunia kujitolea muda na nguvu zake katika kuhifadhi mazingira kama bingwa wa Umoja wa Mataifa wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Aidha amekuwa balozi anayeheshimika na uhifadhi wa mazingira kwa Serikali ya Tanzania, na balozi wa Justdiggit" ilieleza taarifa.

Pia taarifa, ilisema taasisi hiyo, Lead Foundation na Ben Pol wanalenga kuongeza uelewa juu ya kuweka upya mazingira ya Afrika kuwa ya kijani kibichi kwa kuhamasisha upandaji wa miti na kushughulikia suala la mabadiliko ya hali ya hewa linaloendelea kote duniani.




Mratibu wa Taasisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Mazingira (UNEP), Clara Makenya (kushoto), akipokea mche wa mti wa matunda kutoka kwa Mkurugenzi wa Doris Mollel Foundation, Doris Mollel (wa pili kulia), baada kumalizika kwa semina kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi zinavyochangia ongezeko la kuzaliwa kwa watoto njiti na vifo vya wajawazito, jijini Dar es Salaam. Kulia ni Meneja wa Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald ambao ni wadau katika kusaidia uhifadhi mazingira na juhudi za serikali katika sekta ya afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania kuipa Sudan Kusini mbinu za mapato

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA kupitia Chuo cha Kodi (ITA), inatarajia kuwajengea uwezo watumishi wa Mamlaka ya Mapato Sudan Kusini, ili kuongeza mbinu za vyanzo vya ukusanyaji mapato na kukuza uchumi nchini mwao.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Isaya Jairos, amesema kadhalika Tanzania, kuanzia mwezi huu itaanza kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano wa utendaji kazi shughuli za mamlaka hiyo.

Profesa Jairos aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mahafali ya 24 ya chuo hicho yatakayofanyika wiki hii, huku Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Mwigulu Nchemba akitarajiwa kutunuku vyeti 387.

Mkuu huyo wa chuo, alisema wahitimu 387 watatunukiwa vyeti baada ya kuhitimu kozi tofauti ngazi ya shahada, stashahada na astashahada na wanafunzi waliofanya vizuri zaidi katika mwaka wa masomo 2020/2021, kupewa tuzo.

"Chuo cha kodi kinajivunia mafanikio katika kutoa mafunzo ya forodha na kodi. Tayari wanafunzi 5,535 wamepata mafunzo na kuhitimu katika kozi mbalimbali tangu mwaka 2008 hadi 2021.

"Chuo hiki ni pekee hapa nchini na katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, chenye usajili na ithibati ya kudumu kutoa mafunzo ya forodha na kodi kwa wadau mbalimbali," alisema Prof Jairos.

Kadhalika, alibainisha kwamba chuo hutoa mafunzo yanayoendana na mabadiliko ya sayansi teknolojia na uchumi yanayolenga mahitaji ya soko la wataalamu katika nyanja za forodha na kodi nchini, barani Afrika na duniani.

"Chuo kimepata cheti cha kimataifa cha ubora katika kutoa mafunzo ya kodi kinachotolewa na Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO), baada ya kufanya ukaguzi wa usimamizi wa ubora katika shughuli zinazofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," alisema Prof Jairos.

Pia, alisema ITA, kinatoa ushauri wa kuwajengea uwezo watumishi wa TRA, Bodi ya Mapato Zanzibar(ZRB) na mamlaka zingine za mapato barani Afrika.

"Chuo sasa kipo katika makubaliano ya kuwajengea uwezo watumishi wa Mamlaka ya Mapato ya Sudan Kusini na miongoni mwa wahitimu wa mwaka wa masomo 2020/2021, ngazi ya stashahada ya uzamili ni wanafunzi wanne kutoka Sudan Kusini," alibainisha.

Kati ya wahitimu 387, wapatao 140 watatunukiwa Cheti Cha Usimamizi wa Forodha cha Afrika Mashariki, 32 kutunukiwa Cheti cha Uwakala wa Forodha na Kodi, 71 kupewa Stashahada ya Usimamizi wa Forodha na Kodi, 110 watatunukiwa Shahada ya Usimamizi wa Forodha na Kodi na 34 Stashahada ya Uzamili katika Kodi.

# Wanadiaspora wapewa fursa kuchangia maendeleo nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wanaoishi ughaibuni wamerahisishiwa njia ya kushiriki katika maendeleo nchini.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya kuzinduliwa huduma ijulikanayo kama Nyumbani Banking. Huduma hiyo imezinduliwa na Benki ya Stanbic imezindua huduma mpya kwa ajili ya Watanzania wanaoishi ughaibuni. Nyumbani Banking ilizinduliwa kupitia mkutano wa mtandaoni wenye mada Wekeza Nyumbani: Tiketi yako ya kutengeneza utajiri ('Investing back home: a ticket to build wealth), na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akiwa mgeni rasmi, na kushuhudiwa na Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Kevin Wingfield.

Akizungumza wakati wa mkutano huo kwa njia ya video, Mulamula alisema kuwa Watanzania wanaoishi ughaibuni wamekuwa chachu ya maendeleo ya taifa, na ni muhimu kutambua mchango wao katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Uzinduzi wa Nyumbani Banking umekuja wakati muafaka ambapo serikali inalenga kuhakikisha kuwa mchango unaotolewa na Diaspora nchini unatambulika na unatumika ipasavyo kuboresha maisha ya wananchi wenzao nchini.

Naye Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Wingfield alisema wanadiaspora wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi kupitia utumaji fedha na ujasiriamali ambao umeleta maendeleo makubwa na ya kusisimua katika miaka ya hivi karibuni.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja, Omari Mtiga, alisisitiza kuwa Nyumbani Banking ni fursa kubwa kwa wanadiaspora kutumia kujijengea mali nyumbani. Akiongeza kuwa nchi ina fursa kubwa za uwekezaji kutokana na utajiri wake wa asili, utulivu wa kisiasa na uchumi, mazingira chanya ya uwekezaji na huduma ya kibenki sahihi ni chachu ya kutimiza malengo yao.

Kwa muda wa miezi 10 iliyopita, benki ilizungumza na wateja waliopo diaspora juu ya kile wanachotafuta kutoka kwa benki ya nyumbani. Hivyo huduma hii ya Nyumbani Banking imetengenezwa mahususi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wanadiaspora na watapata huduma mbalimbali kama; kufanya miamala, ushauri wa uwekezaji, huduma za bima na mambo mengine. Wakati akielezea huduma hiyo, Meneja wa Benki ya Stanbic, Thereza Majinge, alisisitiza dhamira ya benki hiyo ya kutengeneza suluhu zinazokidhi matakwa ya wateja. Na kwamba wanadiaspora wanaweza kufungua akaunti ya Nyumbani Banking kwa urahisi popote walipo kutumia huduma ya kufungua akaunti mtandaoni na kuendelea kufanya miamala wakiwa huko huko ughaibuni.




Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Diaspora katika Wizara ya Mambo ya Nje na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tagie Daisy Mwakawango (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, wakati wa uzinduzi wa huduma ya Nyumbani Banking, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yahimiza utawala bora ununuzi na ugavi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

OFISA Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, amesema tofauti na zamani, sasa hivi fani ya ununuzi na ugavi ni nyeti kitaasisi na muhimu katika mafanikio ya biashara za kisasa.

Amewataka wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini kuzingatia maadili, uadilifu na weledi katika sehemu zao za kazi.

Aliwaambia wataalamu hao jijini Arusha Jumanne wiki hii kuwa utawala bora na ubunifu ni muhimu ili tasnia hiyo iweze kuchangia kikamilifu maendeleo ya taasisi za sekta binafsi na zile za umma.

Akizungumza wakati wa mkutano mkuu wa kwanza wa mwaka wa Chama cha Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi nchini (APSP) ambapo alikuwa mgeni rasmi, Zaipuna alisema pia mabadiliko ya kisheria yamewafungulia fursa mpya wataalamu hao.

"Nina imani kuwa mtatumia mkutano huu kujadili, kuchambua na kuweka mikakati ya uboreshaji katika fani ya manunuzi na ugavi... nia ikiwa ni kuongeza uadilifu, uaminifu na ufanisi kwenye sehemu zenu za kazi," alisema Zaipuna.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Kimataifa ya Ununuzi na Ugavi (CIPS), alisema suala la maadili na uadilifu linazidi kuwa nyeti kutokana na kuimarika kwa hadhi ya fani hiyo. Zaipuna anakubaliana na mtazamo huo na kuwaasa wataalamu wa ununuzi na ugavi kujiepusha na rushwa. Aidha, aliwataka wataalamu hao kuweka sawa uwiano kati ya mahitaji ya biashara na miongozo ya sheria na kanuni za manunuzi ili waendane na kasi ya mabadiliko na mahitaji kwenye maeneo yao ya kazi.

Katika hatua nyingine, alizindua Bima ya Maisha ya Mkono wa Pole kwa ajili ya wanataaluma wa fani ya Ununuzi na Ugavi na kuwashukuru wana APSP kwa kujiunga na utaratibu huo wa NMB wenye lengo la kuwasaidia wanapokumbwa na janga la kifo.

Alisema benki hiyo inazo suluhisho nyingi bunifu za kifedha kama hizo akitolea mifano ya mfuko wa bima ya afya wa NMB Dunduliza na bidhaa ya akiba ya "Spend to Save".

Mwenyekiti wa APSP, Emmanuel Urembo, aliipongeza NMB kwa kuwa kinara wa huduma za kifedha nchini akisema hilo linathibitishwa na kupata kwake tuzo nyingi za kimataifa za ubora na ufanisi katika shughuli zake.

Alisema umuhimu wa chama chao na thamani ya tasnia hiyo unatokana na ukweli kuwa takribani asilimia sabini ya fedha zinazotengwa kwenye bajeti ya serikali na taasisi binafsi zenye miradi ya maendeleo hutumika kwenye ununuzi wa vifaa, huduma, kazi za ushauri na ujenzi.

## UCSAF, Airtel zapeleka huduma ya 4G kijijini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania imeungana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kupelekea huduma ya mawasiliano ya 4G katika Kijiji cha Matuli Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kwa kuzindua mnara wa mawasiliano.

Mnara huo ambao unatoa huduma ya 4G umejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 350, huku UCSAF ikichangia Sh. milioni 125 kati ya hizo, ambapo mnara huo ulizinduliwa jana na Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji.

Akizungumza baada ya kuzindua mnara huo, Waziri Kijaji aliwashukuru Airtel Tanzania kwa kushirikiana na UCSAF katika kufanikisha kupeleka huduma ya mawasiliano ya 4G katika Kijiji cha Matuli pamoja na vijiji vya jirani vitatu, ambavyo vimekuwa vimekosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

"Wakati tunasherehekea miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania, pia ni muhimu kusherehekea mafanikio ya vijiji vinne vya Jimbo la Morogoro Kusini kwa kufikiwa na huduma ya mawasiliano ya 4G jambo ambalo litawanufaisha wanakijiji zaidi ya 9,000 kwani kuanzia leo watakuwa na uhakika wa kupata huduma bora ya mawasiliano," alisema Dk. Kijaji, huku akipongeza juhudi za Airtel za kupeleka huduma ya mawasiliano kwenye maeneo ya vijijini.

Waziri Kijaji aliongeza: "Kama mnavyojua kampuni ya Airtel Tanzania inamilikiwa na serikali kwa asilimia 49 na UCSAF ni serikali, kwa kushirikiana pamoja kuleta huduma ya mawasiliano hapa Matuli kunaonyesha ni kwa kiasi gani serikali imejitolea kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora ya mawasiliano popote pale walipo."

Mkurugenzi Mtendaji UCSAF, Justina Mshiba, alisema kuwa moja ya lengo kuu ya UCSAF ni kuhakikisha maeneo na hasa ya vijijini yanafikiwa na huduma ya mawasiliano. "Tumekuwa tukishirikiana na kampuni za simu kuhakikisha kuwa tunapeleka huduma ya mawasiliano kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hiyo. Mpaka sasa tushapelekea huduma ya mawasiliano kwa kata 1,068 na bado tunaendelea kwa lengo la kufikisha huduma ya mawasiliano kwa kila Mtanzania," alisema.

Meneja Uhusiano Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, alisema Airtel lengo lake ni kuhakikisha kuwa wateja wake wanapata uhuru na uhakika wa mawasiliano na ndio sababu walijibu haraka baada ya kupata ombi la kujenga mnara huu ambao unatoa huduma ya 4G.

Mmbando aliongeza: "Airtel imekuwa ikiwekeza sana kwenye kupanua wigo wa mtandao wake kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja wake."

Mbunge wa jimbo hilo, Hamis Taletale, aliishukuru Airtel kwa kuungana na UCSAF na hatimaye kufanikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa Kijiji cha Matuli pamoja na vijiji vya jirani.



Ukurasa 14



EWURA yafunguka jinsi inavyojipanga kukabili milipuko moto kwenye makazi



Ukurasa 13

**Aliyebakwa asimulia kovu la hisia linalodumu, somo lililokaa moyoni**

# Chupa plastiki zenye rangi zinavyoumiza vichwa vya wanamazingira vitani, serikali

- Wazalishaji waanika kina cha utata zilivyo
- Sheria yaja; kampuni zaungana kupatia jibu

**Na Romana Mallya**

Ni saa sita mchana katika ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la Daraja la Salander jijini Dar es Salaam. Kwa mbali anaonekana mama wa umri wa makamo akiokota chupa, lakini siyo za aina zote. Anatumia staili ya kuokota kutupia kwenye mfuko aliojitwisha mgongoni.

Hapo nyendo zake zinaacha maswali, kulikoni uchaguzi wake wa chupa anaacha zingine, hata inamvutia mwandishi wa makala hii aliyekuwa katika mandhari hayo, kutaka kujua tofauti hiyo ya uchaguzi wa chupa, baadhi anaziacha, ilhali zinapatikana kwa wingi?

Udadisi huo unapata jibu kutoka kwa mwokotaji huyo, Khadija Yusuph (52), mkazi wa Mwananyamala, anayefafanua siyo aina zote za chupa zinahitajika kiwandani wanakoziuza.

Khadija anasema chupa zisizo na rangi ndiyo zenye soko kubwa kuliko zenye rangi, ndiyo maana kwa kiasi kikubwa zenye rangi zinaendelea kuonekana kuzagaa mtaani licha ya wingi wake.

**WADAU MAZINGIRA**

Baada ya maelezo hayo, udadisi wa Nipashe ulifunga safari hadi iliko asasi isiyo ya kiserikali ya Human Dignity and Environmental Care Foundation (HUDEFO) iliyopo Sinza A, Dar es Salaam, inayohusika na kusafisha mazingira kwenye fukwe, mito, mapango na maeneo mengine.

Mkurugenzi wake, Sarah Pima, anakiri programu yao inayotoa elimu ma kusafisha mazingira, imekutana na tatizo la kusambaa mitaani chupa zenye rangi.


Sarah anasema, hivi sasa wanafanya kazi hiyo katika ngazi ya jamii, wakishirikiana na serikali na watoa uamuzi katika programu yao ya mazingira, ndipo walipobaini siyo chupa zote zinazookotwa na kurejeshwa viwandani.

Anasema kuanzia mwezi Juni mwaka huu walipewa ufukwe wa Coco uliopo Oysterbay na mapango yake walikosafisha na kuwekewa nyenzo za kutupia taka, wakitoa elimu kwa wafanyabiashara wa eneo hilo kuhusiana na utunzaji mazingira.

"Tumeongea na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ambao wao hutoa gari kwenda kuchukua uchafu eneo hilo. Chupa zenye rangi ni tatizo kubwa, zimezagaa maeneo mengi, tumepiga kelele sana," analalamika.

Mkurugenzi huyo anasema huwa wanaangalia aina za taka zinazopatikana kwa wingi kwenye mazingira husika, kisha wanashirikiana na serikali, kuwatembelea wamiliki wa viwanda husika.

"Tulitembelea wamiliki wa viwanda (anavitaja) ambao nao walikiri tatizo la chupa zao kuzagaa mtaani baada ya bidhaa kutumika na waliahidi kuchukua hatua za kuzirejesha, lakini bado tunaziona mtaani kwa wingi," anaeleza Sarah.



Daraja la mbao lililojengwa kwa kutumia chupa za plastiki zilizorejelezwa kiwandani. **PICHA: ROMANA MALLYA**

Anaeleza furaha yake ni kwamba, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, kupiga marufuku kuonekana chupa mitaani baada ya mwezi huu.

Mwanamazingira huyo anafafanua, taka wanazokusanya ufukweni Dar es Salaam, asilimia 80 ni chupa za pastiki na zote wanazitupa katika dampo la Pugu, Dar es Salaam.

**VIWANDA HUSIKA**

Yoyo Chen, ni raia wa China kutoka kampuni ya Sunda iliyoko Dar es Salaam, inayorejeleza bidhaa kwa kutumia mabaki ya chupa za plastiki zilizookotwa.

"Tunataka chupa zisizo na rangi ambazo tunatengeneza nyuzi nyuzi, tunazitumia kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo mito ya ulalia, blanketi (duvet).

"Chupa zenye rangi hatuzitaki, kwa sababu ni ngumu na soko la dunia tunataka malighafi zinazotokana na chupa za plastiki zisizo na rangi. Bidhaa tunazozitengeneza hapa Tanzania tunauza ndani na nje ya nchi, hivyo lazima tuendane na soko la dunia linataka nini," anasema.

Safari ya Nipashe ikafika katika kampuni ya ECOAST Tanzania, iliyoko Tegeta na kukutana na Mkurugenzi wake, Christian Mwijage, anayekubali anatumia chupa za plastiki kutengeneza mbao zisizooza, haziliwi na mchwa na rafiki wa mazingira.

"Kwa miaka mitatu tunafanya kazi hii, kila mwezi tunatumia zaidi ya tani 10 mpaka tani 12 za taka za plastiki na kuzibadilisha kutoa mbao zaidi ya 1,400. Kwa hiyo, unaweza kuona ni miti mingapi ambayo tunaweza kuiokoa," anabainisha.

Kama alivyo mtangulizi wake, Mwijage anaiambia Nipashe wanahitaji zaidi malighafi chupa zisizo na rangi huzihitaji zaidi, kwa sababu ni urahisi kuzirejeleza.

Mwijage anasema, katika kuiunga mkono serikali katika utunzaji mazingira, kampuni yao inatengeneza mbao kwa kutumia mabaki ya chupa wakiamini zingebaki kwenye ardhini, zingekuwa na athari kwa mwanadamu na viumbe vinginevyo.

Anasema, wanatumia bidhaa za plastiki zisizo na rangi kwa sababu ni rahisi kutengeneza na hata kubadilisha kwenda rangi ny-

INAENDELEA UK.12

MAZINGIRA

# Chupa za plastiki zenye rangi zinavyoumiza vichwa vya wanamazingira vitani, serikali

INATOKA UK.11

ingine kirahisi.

"Tani moja ya chupa za plastiki haiwezi kukosa mbao kati ya 100 hadi 120. Tukizungumzia suala la utunzaji mazingira maana yake tunaokoa mpaka hekta tatu za miti ambazo zingekatwa kwa ajili ya mbao," anaeleza.

Anataja soko la bidhaa zitokanazo na mabaki ya plastiki, liko kwenye hoteli za kitalii na kwa nje ya nchi zinauzwa Kenya, Uganda, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) na Afrika Kusini imeonyesha nia ya kuzihitaji.

Mwijage anafafanua, wamenunua mtambo wa kuchakata chupa zisizo na rangi, ili kuiunga mkono serikali kuhakikisha mazingira yanakuwa salama. Elineca Ndowo, Mkurugenzi Mwenza ECOAST, anasema awali walikusanya chupa za plastiki mitaani, lakini sasa wanapata bidhaa kutoka viwandani na kampuni zinazokusanya bidhaa hizo mitaani.

### OFISI YA MAZINGIRA

Ofisa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Hussein Omar, anakiri kuwapo tatizo la chupa nyingi za rangi mitaani. Anafafanua: "Serikali tumeshaanza jitihada, mwanzoni mwa mwaka huu tulikutana na wazalishaji wote wa chupa za rangi lengo tulikuwa tunatafuta tunafanya nini ili kuondokana na tatizo hili."

Ananukuu Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, inayotaka kila anayechafuzi mazingira nchini, kuwajibika na uchafuzi, akisema: "Tuliwaita ili kuwakumbusha wajibu wa kisheria, kwa sasa nchi ipo kwenye mchakato wa kuandaa mwongozo utakaowezesha utekelezaji mzuri wa sheria hii."

Anasema hadi sasa wako katika mchakato kuandaa mwongozo utakaomshurutisha kila anayezalisha taka za namna hiyo, awajibike kuziondoa, huku akigusia kuwapo walioanza kuonyesha jitihada za usafishaji.

Sambamba na hiyo, anasema kuna mwingine unaoitwa 'mwongozo wa punguza, tumia tena, rejeleza' uliotarajiwa kutoka wakati wowote, ukimtaka kila mzalishaji taka na mtumiaji, ahakikishe anapunguza.

Hata hivyo, anatumia mifanikio ya kuigwa akisema: "Cocacola na kampuni nyingine zipo kama tatu, wameunda kitu kinaitwa PRO (Producers Responsibility Organazition).

"Wameunda kampuni hii ambayo itawajibika kwa niaba yao kushughulika na taka zote zinazotokana na bidhaa zao. Bado haijaanza kazi, lakini wapo katika mchakato wa mwisho wa kuanza."

Dk. Omar anasema utafiti mdogo uliofanyiwa na taasisi moja katika ufukwe wa bahari, mito na maziwa umeonyesha tatizo ni kubwa kwa sababu ndani ya saa chache katika ufukwe wenye urefu wa kilomita tatu mpaka tano, unakusanya chupa hadi viroba 150.



Mdau wa mazingira akishiriki kampeni ya ukusanyaji taka za plastikii kwenye ufukwe wa Coco, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**



Dawati lililotengenezwa na chupa za plastiki zilizorejelezwa kiwandani. **PICHA: ROMANA MALLYA**

> **Tunaozalisha bidhaa za plastiki, tumeamua kuunda kampuni ambayo inaratibu uokotaji, ukusanyaji, uchakataji wa bidhaa za plastiki kutoka kwetu tunazalisha.**

### MZALISHAJI AFUNGUKA

Mkurugenzi Mtendaji wa Coca-Cola Kwanza, Tanzania Unguu Sulay, anaeleza baada ya kubaini shida ya uharibifu wa mazingira unaofanywa na chupa zenye rangi wamebuni mbinu ya kukabiliana nayo.

"Tunaozalisha bidhaa za plastiki, tumeamua kuunda kampuni ambayo inaratibu uokotaji, ukusanyaji, uchakataji wa bidhaa za plastiki kutoka kwetu tunazalisha.

"Hii inatupa uwezo wa kutambua ni kiwango gani tumeingiza kwenye mazingira na kiwango gani tumekitoa kwenye mazingira, tukiulizwa swali na serikali siku moja, tuweze kuwe na takwimu sahihi," anabainisha.

Anasema kampuni hiyo ni huru na anawahamasisha wenye viwanda ambao hawajajiunga, washirikiane kama walivyofanya wao.

"Kuanzisha kampuni hii tulifanya katika nchi mbili, Afrika Kusini na Kenya na huko linaendelea vizuri na tutahakikisha tunaboresha pale ambako wenzetu wamefikia,"anasema.

Sulay anasema serikali inawaunga mkono kwa kuwaongoza katika kanuni, mawazo na kuwatia moyo, lengo ni kufanya biashara yenye ustawi kwa mazingira ya taifa kwa kizazi kilichopo na kijacho.

"Vijana ni wengi wapo baadhi wanatumia kuficha vitu katika chupa hizi za rangi, nchi inapiga marufuku pombe ya viroba, lakini kwa chupa hizi unatengeneza mazingira mengine kwa vijana kuendelea kutumia viroba, kwa sababu wanaamini wakiweka humo hazionekani," anabainisha.

Anafafanua: "Kama chupa za plastiki zitabaki mtaani na kushindwa kurejelezwa na kuishia kuchomwa, maana yake tutaharibu anga letu na zikiingia kwenye ardhi ni mbaya zaidi kwa sababu hazionekani.

Anasema ni mara ya kwanza baada ya miaka 60, wamebadilisha chupa ya kinywaji chao Sprite kilichokuwa kwenye chupa ya kijani na kuwa kwenye kifungashio kisicho na rangi.

### WADAU SERIKALINI

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, anasema shida kubwa wanayokutana nayo ni kuzagaa chupa zenye rangi kwenye ufukweni, kwenye maziwa, makorongo na mito.

"Kama alivyoagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, tunaweza kuamua kama nchi, kama tulivyoamua kuondoa vifungashio vya plastiki na ikawezekana," anasema Dk. Gwama.

Bosi wa NEMC anafafanua wameshaandika barua kwa baadhi ya wazalishaji wajiwekee utaratibu wa kukusanya chupa ziwarudie, kwa mujibu wa kanuni kuu ya mazingira ya ukusanyaji taka ngumu.

Anasema, ardhi inapotapakaa chupa au plastiki nyinginezo, ubora wake unaharibika ukigusa viumbe vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Waziri Selemani Jafo, anasema mchango wa urejelezaji ni mkubwa, kwani unawezesha kupata bidhaa nyingine rafiki akiahidi ndani ya miezi 12 kutakiwa na mabadiliko makubwa.

Anawataka wazalisha vinywaji viwandani, wahakikishe wanatumia chupa isiyo na rangi, ili ziweze kurejelezwa viwandani na ikishindikana, anayetoa chupa ya rangi ahakikishe kwa asilimia 100 izikute mtaani awe na mtambo wa kuzirejeleza mwenyewe."

Kimsingi Makubaliano ya Hali ya Hewa ya Paris yaliyofikiwa mwaka 2015, ina miongozo mbalimbali inayotakiwa kutekelezwa na nchi wanachama duniani, ikiwamo Tanzania.

Kwa maana hiyo, tafsiri pana ya chupa zinazotupwa na kuokotwa ndani ya mazingira ya nchi, yanapaswa kuwa na hatua zenye tafsiri za kimazingira, kukabili uchafuzi wawa hali ya hewa nchini na kwa majirani.

Mnamo Oktoba 30 hadi Novemba 11, mwaka huu jijini Glasgow, nchini Scotland kumefanyika mkutano ambao ajenda kubwa ni kujadili athari za mabadiliko ya tabia nchi, inayojumuisha mambo hayo.

Vilevile Oktoba 2, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia, katika Mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa nchini Marekani, alieleza Tanzania haijaachwa kando na kinachotokea katika athari hizo na wanashuhudia kina cha bahari kuongeka na ardhi kumezwa. Alieleza hitaji la ushirikiano kukabili mabadiliko ya tabianchi kwa umma.

AFYA

# Aliyebakwa asimulia kovu la hisia linalodumu, somo lililokaa moyoni

**Na Mwadishi Wetu**

## • Ajabu na kweli, alipewa fursa kusali

KAREN Lina, kwa jina maarufu Princess ni mwanamke mwenye umri miaka 44. Miaka miwili iliyopita alipitia kipindi kigumu cha kutokusahau maishani mwake.

Ni tukio anataja la kubakwa, ambacho hakudhania kwamba kingeweza kumtokea, kwani aliyemtendea hilo ni mtu ambaye hakuwahi kumwona au kumfahamu maishani.

Anaposimulia kisa hicho, bado makovu yaliyompata humjia kwa hisia za uchungu na kero, ingawa sasa ameamua kukubali hali na kusonga mbele.

"Wakati ambao nilipitia kitendo cha ubakaji, nilikuwa nimeishi kwa miezi mitatu tu baada ya kuondoka katika ndoa yangu," anaeleza, akiwa ameondolewa kwenye makazi alikoishi jijini Nairobi.

Anasimulia masaibu hayo ni pale alipoanza maisha ya pekee na ilibidi achukue hatua ya kutembea kwa muda mrefu akielekea eneo la ibada za asubuhi, kama njia ya kufanya mazoezi.

"Nilikuwa nimeishi katika eneo hilo kwa zaidi ya miezi mitatu hivi, kila siku kati ya saa 12 na asubuhi na saa 12.30 ilikuwa nafanya mazoezi yangu. Sikuwahi kuogopa, eneo lile lilikuwa salama kwa hivyo sikuwa na wasiwasi wa kutembea muda huo," anakumbuka mwanadada huyo.

Anasema siku hiyo anaitaja Jumanne, akielekea iliko barabara kuu, ana simulizi yake akifafanua: "Nilikuwa nimeanza kutembea tu niliposikia mtu ambaye alikuwa anatembea kwa kasi nyuma yangu akielekea katika eneo nililokuwa nikienda.

"Niligeuka na kuona alikuwa mwanaume na nikamtaka apite mbele yangu. Lakini alisisitiza kwamba niendelee tu. Ghafla kabla nifahamu ni kipi kilikuwa kinatendeka, niliona upanga kwenye shingo yangu na akasema kwamba nisijaribu kusonga," anasimulia.

Princess anasema udhalimu huo ulifanyika kwa haraka sana. Kwanza anasimulia mkoba aliokuwa ameubeba ulianguka na akaniambia mtu huyo alikuwa anaelekea katika ibada, akiwa radhi achukue chochote alichokitaka ndani ya mkoba wake.

Anasema kutokana na mafunzo ya hapo awali yaliohusu kujilinda wakati wa mashambulizi, alifahamu kwanza sio vizuri kujibizana na mshambuliaji na wakati wote utulivu ulihitajika.

"Mtu aliyekuwa ananishambulia alinieleza kuwa nisijaribu kushindana naye na kuwa ikiwa nitakubali yote atakayo kuwa akisema basi hakutakuwa na mabaya



Karen Lina. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

> **Baadaye, alinitaka nielekee barabara tofauti ambayo haikuwa na watu na hapo nikaanza kuingiwa na hofu.**

yatakayonisibu.

"Baadaye, alinitaka nielekee barabara tofauti ambayo haikuwa na watu na hapo nikaanza kuingiwa na hofu," Princess anaeleza na kwamba wakati huo wote, mtu huyo alimshika mkono na hakutaka kuzungumza naye.

Baadaye alimwelekeza katika nyumba moja iliyokuwa na mlango mwekundu, hapo ndio hofu zaidi ikamwangukia, kwani eneo alilokuwa akipelekwa lilikuwa na giza 'totoro' na mara moja akatakiwa asimame mbele ya mlango huo.

Anasema, tayari mtu aliyemshika mateka alikuwa amechukua mkoba wake na kuanza kupekua ili kubaini kilichokuwa ndani, huku Princes akisimulia alijaribu kumlaghai amekubali kumpa namba yake ya simu ili waanze mawasiliano.

"Muda mfupi baadaye, alinitaka kuvua nguo zangu na hapo ndipo nilihisi wasiwasi zaidi, si kwamba sikusikia amri yake ila nilimuuliza eti umesema nini?

"Akarudia tena. Nilijikuta namweleza anaweza kunipa fursa ya kuomba kwanza. Nilitaka kumshawishi asinibake, nakumbuka nilimweleza kwamba mimi bado sina mume na tunaweza kuwa wapenzi," anasema.

Mama huyo anasema, zote zilikuwa mbinu za kuanza mazungumzo ambazo zingemshawishi kuchukua hatua tofauti.

Mwanadada huyo anasimulia mbakaji alikuwa na nia moja tu na hakuwa na nafasi ya kumsikiliza, ingawa katika mazingira ya ajabu alimpatia fursa ya kuomba kwa dakika chache.

"Kwa maisha yangu yote tangu nikiwa binti nilikuwa naomba Mungu na kumkumbusha kwamba, nisiwahi kujipata katika mikono ya mbakaji, nilidhani kwamba fursa niliyopewa ya kuomba pengine.

"Mwenyezi Mungu angenihurumia na kupigana na mbakaji aliyekuwa tayari kunidhulumu, ila baada ya kumaliza dua yangu alinifanyia kitendo hicho cha kinyama bila kujali," anasema mama huyo, huku akikumbuka kutolewa maneno makali akifokewa ilipofika wakati wa kuvua nguo.

Hakuamini kitendo cha dhuluma ya kingono kingefanyika chini ya dakika chache hizo. Anaendelea:"Uchungu huu ni mwingi hata sasa ninapoongea bado nahisi uchungu wa dhuluma hiyo."

Mbakaji alimruhusu kufanya maombi kabla ya kumtendea unyama na baada ya hapo Princess hakuwa na ujasiri wa kumpigia yeyote simu.

Princess anakumbuka kusimama na kububujikwa na machozi akimuomba Mungu "Nimebakwa nikielekea kwenye ibada na wala sio kwa kilabu, sasa naomba unipe nguvu ya kuelekea kwenye ibada na kuendelea na maisha yangu."

Licha ya mbakaji kumwibia fedha zake, alipata ujasiri wa kumsogelea mhudumu wa bodaboda aliyemsaidia. Wakati huo wote alikuwa anaficha sana kilichomtokea.

Mama huyo anasimulia halikuwa jambo rahisi kulieleza kwa wakuu wa kanisa lake hali kadhalika kwa kina dada ambao walikuwa swahiba zake wa karibu.

Baada ya hapo, hatua za haraka zilifanyika kuwasilisha taarifa polisi na mchakato mzima wa matibabu kutokana na maumivu aliyokuwa nayo.

### BAADA YA UBAKAJI

Anasema maisha baada ya ubakaji hayakuwa rahisi, kwanza kukubali alikuwa ameonwa kingono na hakumfahamu aliyemdhuru.

Hadi sasa mwanadada huyo anasema aliyemtendea ukatili huo hajawahi kukamatwa ikiwa sasa ni miaka miwili baada ya mkasa huo.

Princess anasema imekuwa ni safari ya kila siku ya kutafuta kujisimamia, kujipenda na kujikubali, tangu tukio la kubakwa na kuna harufu na aina ya mavazi na mitindo ya nywele kwa wanaume ambayo hapendi kuyaona kwa wengine, kwani humkumbusha siku hiyo ya unyama.

Anasema alipata ujasiri wa kujitokeza wazi kuzungumzia katika ulimwengu wa wanawake wanaobakwa, ili simulizi yake iwe somo kwa watu wote na hasa wanawake wanaoishi na makovu hayo ya kubakwa.

Princess anasema waathirika wa ubakaji wasiweke siri kitendo cha kubakwa kwani kina athari ya kuwapa karaha na machungu ya kila siku ambayo yamepelekea wengine kupata magonjwa na msongo wa mawazo.

*• Kwa mujibu wa BBC*

MAZINGIRA

# EWURA yafunguka jinsi inavyojipanga kukabili milipuko moto kwenye makazi

• Petroli kwenye madumu shida inayojitegemea

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UPO ushuhuda wa matukio mengi ya majanga ya moto yanayosababisha uharibifu mkubwa wa mali, ikiwamo kugharimu maisha ya watu na baadhi yao wakipata ulemavu wa kudumu, hata kuangukia hata kuwa ombaomba mitaani.

Hakika, kuunguliwa nyumba au mali ni jambo baya ambalo watu hawapendi liwatokee na kuna wakati majanga ya moto yanasababishwa na wananchi kuishi na vitu hatari, kama vile mafuta ya petroli au dizeli.

Pia janga la moto linatajwa kuchangiwa na mazingira, hali kadhalika miundombinu duni ya majengo kwa sababu ya ama kukosa elimu au uhaba wa pesa.

Kuna wanaotumia vifaa duni wakati wa kuweka umeme kwenye nyumba, hata inapowatokea tatizo la nyumba kuwaka moto.

Hata hivyo, kuna wakati watu wanawasha vibatari, mishumaa na sigara ndani ya nyumba. Ni hali inayojitokeza kwa wafanyabiashara wanaouza mafuta ya taa, petroli na dizeli kinyemela kwenye makazi yao, vitu vinavyosababisha janga la moto.

Uwapo wa mazingira zaidi ya moto katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, zaidi ni ile itokanayo na mafuta ya taa, diseli na petroli kuungua ndani ya nyumba vijijini, Mamlaka ya Udhibiti Nishati na Maji (EWURA), imesema imejipanga kuanza kuyadhibiti majanga hayo kwa kufanya msako.



Mafuta yakiwa kwenye madumu.

> Tutaendesha msako katika mikoa ya Shinyanga na Geita, ili kuwabaini wafanyabiashara wote wanaouza mafuta kwenye chupa za maji mbele ya nyumba na maduka yao ya biashara, kwa sababu kufanya hivi ni kwenda kinyume na maelekezo ya EWURA.



Wezi wa mafuta kwenye malori, hali inayotajwa kuhatarisha matukio ya moto. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MENEJA KANDA ZIWA

George Mhina, Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, anasema wamejipanga kuanza msako wa kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara wanaouza mafuta ya taa, dizeli na petroli bila ya kuwa na leseni, ili kudhibiti matukio ya moto yanayotokana na biashara hiyo.

Anasema katika hilo, watashirikiana na wadau wa nishati na viongozi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, ili kuangalia namna bora ya kutatua kero hiyo katika sekta ya mafuta na gesi, ambayo imekuwa ikiripotiwa na wananchi hususani maeneo ya pembezoni mwa mji yaani vijijini.

Mhina anasema, mikoa ya Kanda ya Ziwa inaongoza kwa matukio ya nyumba kuwaka moto unaosabababishwa na uhifadhi wa mafuta ya petroli na dizeli kinyemela kwenye makazi, inayosababisha mali za watu kuteketea, wananchi kupata ulemavu na vifo visivyo vya lazima.

"Tutaendesha msako katika mikoa ya Shinyanga na Geita, ili kuwabaini wafanyabiashara wote wanaouza mafuta kwenye chupa za maji mbele ya nyumba na maduka yao ya biashara, kwa sababu kufanya hivi ni kwenda kinyume na maelekezo ya EWURA. Hivyo, wajisalimishe wenyewe kabla msako haujaanza," anafafanua Mhina.

### LESENI ZA EWURA

Mhina anasema, EWURA inatoa leseni kwa wafanyabiashara wanaomiliki vituo vya mafuta pekee, ambao wamekidhi vigezo vya kisheria na daima hawaruhusiwi wanaouza kwenye mapipa, madumu na chupa za maji, akiwa na angalizo maalumu hasa wanaofanya hivyo, maeneo ya vijijini.

Anataja moja ya sababu ya kuanza msako huo ni kuwaondoa wafanyabiashara wanaouza mafuta ya petroli na dizeli kwenye chupa za maji na mapipa, ili kuondoa majanga ya moto yanayotokea kila mara, hata kusababisha wananchi kupata vilema vya kudumu.

### UJENZI VITUO VIJIJINI

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA makao makuu, Wilfred Edwin, anasema kwa sasa upo utaratibu unaowataka wamiliki wa vituo vya mafuta mjini, kuhakikisha wanajenga vituo vingine husunsani vijiji ili kudhibiti wimbi la wauzaji wa mafuta wasiokuwa na leseni.

Nishati ya mafuta inatakiwa kuuzwa kwa utaratibu unaokubalika, hivyo EWURA imeamua kuja na mpango mahsusi unaowataka wamiliki wa vituo vya mafuta kuvijenga vituo hivyo pembezoni mwa miji, ili kukidhi mahitaji ya mafuta kutokana na kushamiri usafiri wa bodaboda.

Anasema, EWURA inawakaribisha wafanyabiashara wenye nia ya kuwekeza katika biashara ya mafuta, ili kuimarisha upatikanaji nishati ya huduma ya mafuta vijijini, ambayo umekuwa mgumu kutokana na shida ya miundombinu ya barabara, hususani kipindi cha mvua.

Pia anaainisha suala la uwekaji vinasaba katika mafuta ya taa, petroli na dizeli kabla ya kuingia sokoni, kumesaidia kupunguza uchakachuaji nishati hiyo kwa asilimia 80, hivyo imepunguza malalamiko yaliyokuwa yanawasilishwa kila mara kwa EWURA ya kuwapo 'mafuta machafu.'

### UDHIBITI WA UBORA

Moja ya majukumu ya msingi ya EWURA, ni kuhakikisha wafanyabiashara ya mafuta wanafuata sheria, kanuni na kukidhi viwango vya ubora katika utoaji huduma za mafuta nchini.

Kwa mujibu wa Edwin, sheria zinazosimamia EWURA, pia petroli zinaipa nguvu za kiufundi, kiuchumi na kiusalama, ili kuhakikisha wanatoa huduma yenye ubora na viwango vinavyostahili.

Anasema, wamekuwa wakikagua kila vituo vya mafuta, maghala ya kuyahifadhi na katika magari ya kusafirishia mafuta, ili kujiridhisha endapo uendeshaji biashara ya mafuta unazingatia masuala muhimu ya kiufundi na kiusalama.

Lingine analolitaja Edwin, ni kwamba ukaguzi huo unafanyika kwa kupima wingi wa vinasaba katika mafuta ya soko la ndani ili kujiridhisha hakuna uchakachuaji, udanganyifu au ukwepaji kodi za serikali na wanaobainika kukosea wanachukuliwa hatua za kisheria.

### WADAU & WAFANYABIASHARA

Julius Chagama, mdau na mtumiaji mafuta ya petroli, anaiomba EWURA kuwataka wamiliki wa vituo vya mafuta kuweka pampu nyeupe, ili wateja waweze kuona mafuta yanaoingia kwenye vyombo vyao vya moto na kupunguza malalamiko ya kuibiwa mafuta.

Anasema, kuna baadhi ya vituo vya mafuta mjini Kahama vimekuwa vikilalamikiwa na wateja kwamba vinawaibia mafuta, akiwa na mtazamo kama pampu zao za mafuta zingekuwa zinaonyesha mithili ya kioo, ingepunguza malalamiko ya kuibiwa.

Mfanyabiashara wa mjini Kahama, Omary Juma, anaomba halmashauri kupima maeneo kubainisha paliko wazi, nyumba za ibada na barabara, ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza, pale watakapoanza ujenzi wa vituo hivyo.





## Kibano cha TBS kwa w/biashara wadanganyifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewaonya wafanyabiashara wanaohariri tarehe za mwisho wa muda wa matumizi ya bidhaa kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Akizungumza wakati wa mahojiano jijini Dodoma, Ofisa Usalama wa Chakula wa TBS, Deus Deule, alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kuhariri tarehe za muda wa matumizi ya bidhaa ambazo muda wake umeisha Ili bidhaa hizo ziendelee kuwa sokoni. Hivi karibuni TBS wakati wa zoezi la kuteketeza bidhaa za chakula navipodozi sisizo na ubora zenye thamani ya Sh. milioni 26.4.

Bidhaa zilizoteketezwa zimetokana na kaguzi zilizofanyika kwenye maeneo mbalimbali ya biashara ikiwamo maduka, maghala, hoteli, na stoo zilizoko katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma na Singida ambazo zinaunda kanda ya kati kwa TBS, Deule, alisema ni marufuku kwa wafanyabiashara kuhariri tarehe za mwisho za muda wa matumizi ya bidhaa na ukaguzi unaendelea kufanyika ili kubaini wanaofanya vitendo hivyo.

Alisema wanaobainika hutozwa faini kwa kujibu wa kanuni za ada na tozo za mwaka 2021, ambapo kiwango cha faini kinaanzia Sh. 500,000.

Katika zoezi hilo jumla ya kilo 4,056 zenye thamani ya Sh. 26,448,500 zimeteketezwa ikijumuisha bidhaa za chakula na vipodozi zilizoisha muda wa matumizi, zenye viambata simu na zile ambazo tarehe za mwisho wa tarehe za matumizi zimehaririwa.

Alisema uwepo wa bidhaa zilizoisha muda wa matumizi na zile zenye viambato sumu zinaathiri uchumi wa nchi pomoja na afya za watumiaji na bidhaa za chakula zilizoisha muda wake na zile ambazo tarehe za mwisho wa matumizi zimehaririwa zinaathiri upatikanaji wa virutubisho vinavyotegemewa vinaweza kusababisha magonjwa ya muda mfupi na mrefu ikiwamo saratani.

Deule alisema kwa upande wa vipodozi hasa vile vyenye sumu, athari zake ni za muda mfupi na mrefu ikiwamo kuathirika ngozi, macho, mfumo wa uzazi kwa kinamama, ukuaji kwa watoto na magonjwa ya saratani hasa ngozi.

# Maadhimisho miaka 60 uhuru kuzinduliwa leo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kuzindua kitaifa sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara katika eneo la mji wa kiserikali Mtumba jijini Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alibainisha hayo jana wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya uzinduzi wa sherehe hizo kitaifa.

"Nchi yetu inatarajia kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara ifikapo Desemba 9, mwaka huu, mkoa wa Dodoma makao mkauu ya nchi umepewa heshima na dhamana ya pekee ya kuandaa sherehe za kitaifa za uzinduzi wa maadhimisho hayo ya miaka 60, ambazo zitafanyika katika eneo la mji wa kiserikali Mtumba," alifafanua Mtaka.

Alisema, katika uzinduzi huo mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na maandalizi yote muhimu kwa ajili ya sherehe hizo yamekamilika.

"Sherehe za uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru zitaanza saa 12:30 asubuhi zikiambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo uzinduzi wa ujenzi wa ofisi za wizara awamu ya pili zinazojengwa katika mji wa serikali Mtumba," alisema Mtaka.

Aliongeza kuwa shughuli nyingine ni uzinduzi wa huduma za kijamii katika mji huo wa kiserikali ikiwa ni pamoja na uwekaji wa jiwe la msingi la kituo cha polisi chenye hadhi ya daraja la kwanza.

"Pia Waziri Mkuu Majaliwa atafanya ukaguzi wa barabara za lami za mji wa serikali Mtumba zenye jumla ya kilometa 51.2 ambazo ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 85,"alisema Mtaka.

Vilevile, Waziri Mkuu Majaliwa atafanya ukaguzi wa jengo la kitega uchumi la Halmashauri ya Jiji la Dodoma lililoko katika mji wa serikali Mtumba.

Alisema kutokana na kutambua umuhimu wa maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru serikali ilitoa maelekezo na mwongozo wa kufanyika kwa shughuli mbalimbali za maendeleo, uchumi na biashara, michezo na kijamii hadi siku ya kilele cha Desemba 9.

"Sisi kwenye mkoa wa Dodoma tulikuwa na maonyesho ya wafanyabiashara na wajasiriamali wa mvinyo, michezo mbalimbali, zoezi la kusaini mikataba ya ujenzi wa miradi ya maendeleo, mashindano ya isha kwa shule za msingi na sekondari,"alisema.

Kadhalika, Mtaka alisema wanatarajia kuwa na makongamano ya kuelekea miaka 60 ya uhuru yakiangazia masuala ya kilimo cha mazao ya kimkakati katika mkoa wa Dodoma.

"Aidha, makongamano pia yataangazia masuala ya upatikanaji wa ardhi na makazi nafuu kwa kaya za kipato cha chini,"alisema.

Hata hivyo, alitoa wito kwa taasisi zote za serikali, binafsi na makundi mbalimbali na wananchi wote wa mkoa wa Dodoma na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi katika uzinduzi huo.



Wanachama wa Chama cha Afya ya Jamii Tanzania, wakimsikiliza aliyekuwa Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Gabriel Upunda (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 38 wa Mwaka, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Serikali yaanika mafanikio utalii miaka 60 ya uhuru

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa katika miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika imeimarisha utalii kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mikakati ya kukuza vivutio mbalimbali vya utalii.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta hiyo kwa kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Masanya alisema vivutio hivyo ni pamoja na hifadhi za wanyama pori, maporomoko ya maji, milima, misitu ya mazingira asilia, utamaduni, fukwe na malikale.

Alisema sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla katika nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania.

Aidha, alisema kuongezeka kwa idadi ya watalii na mapato ni moja ya mafanikio ya kujivunia kutokana na juhudi za serikali za kuendeleza na kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii nchini.

"Idadi ya watalii wanaoingia nchini kutoka katika nchi mbalimbali duniani imeongezeka kutoka 9,847 mwaka 1960 hadi kufikia watalii 1,527,230 mwaka 2019, kumekuwapo na ongezeko la mapato yatokanayo na watalii kwa mfano mwaka 1995 mapato yalikuwa Dola za kimarekani milioni 259.44 ambapo yaliendelea kuongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019 kabla ya ugonjwa wa UVIKO-19," alisema.

Kadhalika alisema kutokana na jitihada za serikali katika kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 idadi ya watalii imeanza kuongeza kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 hadi kufikia 716,169 mwezi Oktoba mwaka huu.

Kadhalika, alisema kuwa Tanzania imejaaliwa kuwa na maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu na nyuki, malikale yenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi.

Vilevile, alisema kuwa mchanganuo huo unatokana na uhifadhi wa mifumo ya ikolojia unaokidhi matakwa ya kimazingira, kijamii na kiutamaduni, kitaifa, kikanda na kimataifa.

Aidha, alisema maeneo ya maliasili yanatoa huduma za maji kwa matumizi mbalimbali makazi ya wanyamapori na viumbe wengine, uchavushaji, uhifadhi wa udongo, ufyonzaji wa hewa ukaa (carbon) hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Maliasili, malikale na utalii ni miongoni mwa sekta za uchumi nchini ambazo zinatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa na kuendeleza ustawi wa maisha ya wananchi kupitia ajira, chakula, tiba na vifaa vya ujenzi.

Sekta hii inatoa malighafi za viwanda vya kuchakata ngozi, kutengeneza mapambo na kusindika nyamapori na kujenga umoja wa kimataifa hivyo hii sekta ikisimamiwa ipasavyo itatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi hususani katika miaka mengine ijayo," alisisitiza.





# Waziri Mkuu asisitiza tahadhari corona

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kuchukua tahadhari za kutosha ili kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa corona ambao umekuwa tishio duniani.

Majaliwa alisema hayo jana wakati akizungumza na wajasiriamali wanaofanya shughuli zao eneo la uwanja wa ndege wa zamani jijini Mbeya ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo jijini hapa.

Alisema wananchi wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari madhubuti katika kukabiliana na corona ili kuhakikisha ugonjwa huo hauingii tena nchini.

"Kila mwananchi kwa nafasi yake ahakikishe anachukua tahadhari kukabiliana na ugonjwa huu wa corona. Kila mmoja ana maumivu yake, tumepoteza ndugu, jamaa na marafiki, hivyo ni muhimu kuhakikisha maambukizi mapya hayafiki nchini kwetu," alisema Waziri Mkuu.

Aliwasisitiza wataalamu wa afya nchini kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kupata chanjo ya corona sambamba na wao kuwa mstari wa mbele kuchanja ili kujenga kinga dhidi ya maambukizi.

Katika kukabiliana na ugonjwa huo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema serikali imeimarisha mikakati ya kupambana na wimbi la nne la corona.

Alisema tangu kuripotiwa kwa ugonjwa huo mwaka 2019, hadi Novemba, mwaka huu, watu 731 wamepoteza maisha na kwamba watu 26,273 walithibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema zaidi ya watu 100 walipata chanjo katika hospitali hiyo na kwamba wanaendelea kuhamasisha wananchi kuendelea kuchanjwa.



Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo (kushoto), akizungumza na wafanyabiashara wa Mkoa wa Ruvuma, akiwa ziarani mkoani humo jana, yenye lengo la kupata taarifa ya tathmini kuhusu maadili na utoaji huduma kwa walipakodi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge apigia debe ajira walimu maalum

Na Grace Mwakalinga, CHUNYA

MBUNGE wa Lupa, Masache Kasaka, ameomba serikali kuajiri walimu wanaofundisha watoto wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha watoto wenye ulemavu katika Shule ya Msingi Kibaoni kupata elimu bora.

Kasaka alitoa ombi hilo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu upatikanaji wa huduma kwa watoto wenye mahitaji maalum katika shule hiyo.

Alisema licha ya serikali kutenga zaidi ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari wilayani hapa bado kuna uhaba wa walimu wa lugha za alama.

"Kuna uhaba mkubwa wa walimu wanaofundisha watoto wenye mahitaji maalum katika shule ya Kibaoni. Watoto wetu wenye ulemavu wa viungo, mtindio wa ubongo, watoto wenye ulemavu wa kusikia wanapata shida. Hakuna miundombinu rafiki wala vifaa vya kujifunza na kujifunzia," alisema Masache.

Hata hivyo, alisema uwapo wa shule jumuishi umechangia kuondoa unyanyapaa kwa watoto na kuhamasisha wazazi kuwapeleka watoto shuleni badala ya kuendelea kuwaficha ndani.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alisema walilazimika kuanzisha shule hizo ambazo hazikuwa rasmi kwa ajili ya watoto wenye ulemavu ili wazazi wapate msukumo wa kuwapeleka shule watoto wao na kwamba kwa mwaka huu, wanafikiria kutenga bajeti kutoka wizarani ili kusaidia shule hizo.

Alisema kutokana na uhitaji mkubwa kwa wilaya, wameanza mikakati ya kuanzisha shule nyingine ya watoto wenye ulemavu katika Mji wa Makongolosi.

# NACOPHA yaishukuru serikali ugawaji wa ARV

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

BARAZA la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), limeishukuru serikali kuendelea kutoa dawa za kufubaza makali ya Virusi vya Ukimwi (ARV) na kwamba hatua hiyo imesaidia kuimarisha afya zao.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Leticia Maurice, alisema hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya.

Alisema serikali imewasaidia Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) kusambaza dawa kwenye vituo mbalimbali vya afya na kusaidia watu hao kupata dawa hizo kwa uhakika.

Maurice alisema baraza linaunga mkono mkakati wa serikali katika kufikia 95 tatu ambazo zinalenga kutokomeza maambukizi ya Ukimwi kwa kuwakinga wengine na kuhakikisha wanaendelea kuimarisha umoja na utengamano kupitia majukwaa yao.

Alisema katika kuhakikisha baraza hilo linafanya kazi kwa ufanisi, wameanzisha mabaraza 180 yakihusisha wanawake na vijana na kwamba WAVIU 600,000 wamejiunga kwenye baraza hilo.

Moaurice aliwahamasisha wananchi kuendelea kupima afya zao na kuishi kwa malengo ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Pia alisema baraza linakabiliwa na tatizo la unyanyapaa, ukatili wa kijinsia kwa kuwa linachangia kasi ya maambukizi ya VVU.

Aliongeza kuwa kamati za kupambana na Ukimwi kuanzia ngazi za vijiji hadi wilaya zimesaidia kuongeza mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema maadhimisho ya Ukimwi mkoani hapa yamekuwa na mafanikio makubwa ikiwamo wajasiriamali kujiongezea kipato.

Mafanikio mengine ni kuwezesha wanawake 146 waliofanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na ya wananchi 1,172 wamejitokeza kupima maambukizi ya VVU na kati yao waliokutwa na maambukizi ni 129 sawa na asilimia 2.5.

"Sambamba na hayo, kumekuwa na mwitikio mkubwa kwenye uchanjaji wa chanjo ya corona. Wengi wamejitokeza kupata chanjo hiyo muhimu kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, hivyo kama mkoa tunashukuru sana kwa heshima hii tuliyopewa na kama itawapendeza waratibu tupewe tena fursa hii mwakani," alisema Homera.



## Sekta binafsi yapewa nafasi kwa uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Thabit Idarous Faina, amesema serikali haina uwezo wa kuajiri vijana wote.

Hata hivyo, amesema serikali inatengeneza mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza kuwasaidia vijana ili kupata fursa za kujiajiri.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na ujumbe wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) uliofika ofisini kwake, Vuga kujitambulisha na kutambulisha mradi wa kukuza biashara ya Africa Franchising Accelerator (AFRAP) visiwani hapa.

Thabit alisema licha ya serikali ya Zanzibar kuahidi kutoa ajira 30,000 kwa vijana, ajira hizo hazitatolewa na serikali pekee badala yake inatengeneza mazingira wezeshi ya kujiajiri na wafanyabiashara wengi kuwekeza hatua itakayozalisha ajira hizo. Aliwataka wafanyabiashara wa Zanzibar kutojifungia ndani badala yake watoke na kuziangalia fursa zilizoko kwenye eneo lao ili kuwa chachu ya mabadiliko na kukuza uchumi.

Mkurugenzi wa Programu ya Maendeleo ya Biashara wa TPSF, Damas Mgashe, alisema kupitia mradi huo wanasaka kampuni 90, kati ya hizo 25 kutoka visiwani Zanzibar ambazo zitaendelezwa kibiashara kufikia soko la kimataifa.

Alisema nia ni kusaidia na kulea biashara ndogo na za kati 90 za kiasili na kubadilisha waendeshaji wadogo kuwa chapa za biashara za kimataifa.

"Huu ni mfumo ambao unapewa leseni kutoka kampuni ambayo imeshajijenga kimataifa kwa hiyo unaendesha biashara zako kupitia mfumo huo," alisema.

Pia alisema kupitia mfumo huo wanataka kujenga chapa ndogo kama mafundi selemala na mamalishe ambao wataunganishwa pamoja kulingana na kazi zao ili iwe rahisi kuwezeshwa na kupanua biashara zao.

Mshauri Mwelekezi wa AFRAP, Wambugu wa Gichohi, alisema mfumo huo unatumika sehemu nyingi dunia lakini kwa Tanzania na Afrika dhana ya matumizi ya mfumo huo bado haijajulikana kwa wafanyabiashara jambo linalowafanya washindwe kukuza biashara zao.

# TAMWA yabaini mazingira mazuri kwa wanawake katika siasa, uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amesema mazingira ya kisiasa nchini kwa sasa yanatoa fursa kwa wanawake wengi kuwa viongozi wa serikali na taasisi binafsi.

Amesema hatua hiyo inatokana na Tanzania kuongozwa na Rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan.

Aliyasema hayo jana katika Ofisi za TAMWA, Tunguu nje ya mji wa Zanzibar wakati akizungumza na viongozi mbalimbali kutoka vyombo vya habari na wawakilishi wa asasi za kiraia.

Dk. Mzuri alitoa kauli hiyo baada ya uwasilishwaji wa ripoti maalumu iliyolenga kwa kiasi gani baadhi ya vyombo vya habari vinavyowaandika wanawake katika nafasi za uongozi visiwani Zanzibar.

Alisema kwa mazingira yaliyopo hivi sasa, ni wazi kuwa nchi imefunguka na fursa zaidi za wanawake wengi kuwa viongozi, hivyo wanachopaswa ni kujizatiti na kuwa tayari kugombea nafasi hizo.

Kwa mujibu wa Dk. Mzuri, ushiriki wa wanawake katika nafasi hizo si jambo la kuonekana kuwa kikwazo bali ni matakwa ya dunia yenye dhamira ya kuleta usawa kwa watu wote, hivyo hakuna sababu mwanamke kuachwa nyuma.

Kutokana na hali hiyo, alitoa wito kwa jamii hususani wanandoa kuacha dhana potofu yenye lengo la kumkandamiza mwanamke kutokuwa kiongozi kwa baadhi ya wanandoa kudai wanawake wanapokuwa viongozi hubadilika na kukataa ndoa zao za awali.

Dk. Mzuri aliwataka viongozi wa vyombo vya habari kuhakikisha wanatoa kipaumbele zaidi pamoja na kuwa na sera maalumu ambayo itawawezesha wanawake wengi kuripotiwa habari zao kila siku.

Awali, akiwasilisha ripoti ya utafiti, mkufunzi wa masuala ya habari Dk. Abubakar Rajab, alisema utafiti huo mdogo ulijikita kwa magazeti mawili ambayo ni la Mwananchi na shirika la magazeti ya serikali, Zanzibar Leo.

Dk. Abubakar alisema kwa kipindi cha Januari hadi Agosti, utafiti huo uliolenga kutazama habari mbalimbali zilizowagusa viongozi wanawake kwa miezi minne na walitazama nakala 120 katika ya magazeti hayo kuhusu habari ambazo zimeandikwa kuhusu viongozi wanawake ni 159 na zote zilizobakia zilijikita kwa upande wa wanaume.

Alisema kwa mazingira hayo, bado kuna tatizo kwenye vyombo vya habari kutokutoa fursa zaidi kwa wanawake jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa na wasimamizi wa vyombo hivyo kubadili mtazamo na kutoa fursa zaidi kwa wanawake kwenye vyombo vyao.

Akichangia uwasilishwaji wa ripoti hiyo Mwenyeki wa Wanaume wa Mabadiliko, Mohamed Jabir, alisema vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuwaandika wanawake na wao ndio watu ambao wanakabiliana na changamoto kubwa katika harakati za kisiasa.

Mhariri wa Gazeti la Zanzibar Leo, Ramadhan Makame, alisema wameuchukua utafiti huo kama changamoto na kuahidi kuzifanyia kazi hoja zilizojitokeza katika kipindi kifupi kijacho. Alisema ni imani yake kuwa utafiti kama huo ukifanyika tena mwakani, utakuwa na matokeo mazuri zaidi.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman (wapili kushoto), akiangalia bidhaa kutoka kikundi cha ujasiriamali cha Shimmer kutoka Mbweni Zanzibar, kabla ya kukabidhi ruzuku kwa vikundi vya vijana wajasiriamali, huko Mazizini, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sababu ukosefu ajira vijana bayana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema bado kuna tatizo la upatikanaji wa ajira kutokana na sababu tofauti ikiwamo ukosefu wa stadi na maarifa ya kuwezesha vijana kuajirika.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar wakati wa hafla ya utoaji wa ruzuku kupitia mradi wa Feed the Future Tanzania - Advancing Youth (Inua Vijana), unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo la USAID ambao umegharimu Dola milioni 1.1.

Othman alisema kupitia mradi huo, vijana wengi wamejitambua na kuwa na uwezo wa kuingia katika soko la ajira wakiwa wenye uwezo na wanaojiamini.

Aliipongeza serikali ya Marekani kupitia USAID kwa ufadhili mkubwa wa kifedha na kiutaalamu unaolenga kuwawezesha vijana kujitambua kama sehemu muhimu ya maendeleo ya jamii na katika harakati za kujikwamua kiuchumi.

Kwa mujibu wa Othman, hilo ni jambo muhimu kutokana na ukweli kwamba ruzuku hizo zimelenga mahali penyewe, hivyo imekuwa rasilimali.

Alisema fedha hizo ni muhimu katika kusaidia kutatua tatizo la ajira kwa vijana hasa wale wanaoishi vijijini kwa kuunganishwa na fursa za mnyororo wa biashara za kilimo na kupatiwa mafunzo stadi ya kazi za ujasiriamali, uongozi, afya ya uzazi na stadi za maisha na kuwataka vijana hao kujitahidi kuongeza kipato, kufanya uamuzi na kupanga mipango bora ya maisha.

Othman alisema anatambua kwamba mbali na Feed the Future Tanzania - Advancing Youth (Inua Vijana), serikali ya Marekani imekuwa mshirika mkubwa wa serikali ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika ufadhili na utekelezaji wa miradi mingi ya kimaendeleo.

Alisema anathamini na kutambua mchango wa serikali ya Marekani katika kuleta ustawi wa watu kwenye maeneo mbalimbali yakiwamo afya, elimu, maji, miundombinu na hasa hasa maendeleo ya vijana wa kike.

Makamu wa Rais aliyaasa mashirika 15 yaliopatiwa ruzuku kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa, ili matokeo ya kweli kupitia kwa walengwa na wanufaika wa ufadhili huo kupatikana.

"Wafadhili pamoja na serikali ya Zanzibar tunaamini fedha hizi ni nyingi na zinaweza kuleta matokeo ya maendeleo makubwa kwa vijana wetu," alisema na kuwataka wajasiriamali hasa vijana kuzalisha bidhaa zenye ubora zinazohimili ushindani wa soko la biashara nchini.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri, alisema serikali ya Marekani imejitolea kusaidia vijana wa vijijini wenye umri wa miaka 15-35 kujihusisha na biashara ya kilimo na minyororo mingine ya thamani vijijini na kuongeza fursa zao za kiuchumi na kukuza uongozi na maisha bora.

Alisema awali USAID walikutana na vijana 45 walionufaika ambao walionyesha jinsi wanavyosindika bidhaa zao zikiwamo mtindi, jamu za matunda, asali, vyakula na unga wa moringa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOETELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **ASHERI KATARAIA MJUNGU** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya **RAV 4** lenye namba za usajili **T 419 CRM,** Injini namba **3S2013540** na Chassis namba **SXA110118899.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/568074/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0752905354.**

116595602

## KUPOETELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **KAMAYUGI SYPHORIAN KAMAYUGI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya **Toyota Mark II** lenye namba za usajili **T 626 BTX,** Injini namba **4SEAA6251** na Chassis namba **SX805066251.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/568077/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0752905354.**

116595702

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**KIGOMA**
**.........................................................................**
**MAHALI :KIGOMA**

**MAOMBI NA 43 MWAKA 2021.**

**ALTEMO VYAMUNGU......................................MW**

**DHIDI YA**

**RAMADHANI IDD,FRANK EMILY MTEGANO........................................MJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA........ RAMADHAN IDD,FRANK EMILY MTEGANO.**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 06 mwezi 12 mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya muheshimiwa F.Chinuku Mwenyekitiwa baraza Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
AMRI hii metolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili
Leo tarehe 26 mwezi wa 10 mwaka 2021.

MWENYEKITI

116595802

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**MARIAM SIGSBERT MAKORONGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 594 CXW.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBA/RB/560323/2021**

116596002

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT COURT OF MOMBA**
**AT CHAPWA**

**CIVIL CASE NO.8 OF 2021**

**ELIZA ADAMSON KILINGO........................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**WILE MWENSI LWINGA...........................DEFENDANT**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 civil procedure Code)**

**TO : WILE MWENSI LWINGA**

WHEREAS the above named Plaintiff has instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the point;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you.If there is more than one plaintiff,additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs.If there are more defendants than one and the defence is not joint defence,there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statement of defence within the time specified,the court may pronounce judgement against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon.P.J.RUPIA-RM Judge/Magistrate on the 03 day of 12,2021 at 07:30 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 26 day of 11,2021.

RESIDENT MAGISTRATE
MOMBA

116596102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **DAUDI IBRAHIMU MAKONGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya MTR yenye namba za usajiri **MC 880 APX.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **TAN/RB/561511/2021**

116596402

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**

**Kituo Cha Mjini Mkoa wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na 329/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU LETICIA KASIMIR MASANJA WA AREA FIVE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NINE ZAKARIA KANYEKA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 08 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .
**Zingatia**
Endapo Kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa Leo 01 Mwezi 12 Mwaka 2021**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116596902

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## SIKU YA UKIMWI DUNIANI:

# Milioni 35 wamefariki, COVID-19 inatatiza vita dhidi ya Ukimwi

**Geneva,** USWISI

WATAALAMU wa afya na wanaharakati wa haki za wanaougua ugonjwa wa Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI), wamesema janga la COVID-19 limezifanya juhudi za kupambana na UKIMWI kutengwa kando na malengo ya kuutokomeza kupuuzwa.

Ripoti mpya ya Shirika la Afya Duniani Barani Ulaya (WHO-Europe), iliyochapishwa mjini Geneva, inasema janga la virusi vya corona, limesababisha idadi ya watu wanaokwenda kupima VVU kushuka kwa kasi, na kuongeza uwezekano wa maambukizo mapya kusambaa na watu wengi kuugua ugonjwa huo.

"Watu waliokwishaambukizwa virusi vya UKIMWI na ambao hawatibiwi wana hatari zaidi ya kuambukizwa virusi vya corona na kuvisambaza kwa wengine," ilisema ripoti hiyo iliyochapishwa kwa ushirikiano wa WHO-Europe na Taasisi ya Kuzuia na Kudhibiti Maradhi ya Ulaya, ECDC.

"Maambukizi mapya ya VVU yamekuwa yakiongezeka kwenye eneo la Ulaya." Ilisema sehemu moja ya ripoti hiyo iliyochapishwa kuadhimisha Siku ya Ukimwi Duniani, jana.

Kwa mujibu wa wataalamu walioshiriki kuandaa ripoti hiyo, kusambaa kwa UKIMWI kuna athari za moja kwa moja kwenye usambaaji wa maradhi mengine.

Baadhi ya wanasayansi wanaamini kuwa aina mpya ya kirusi cha Omicron, kimetokana na mgonjwa wa VVU, kwani mtu mwenye VVU akipatiwa matibabu ya kiwango cha chini, anaweza kuwa na mfumo wa kinga usio na uwezo. Pia anaweza kuufanya mwili wake kuwa mahala, kirusi kinaweza kujibadilisha sura zake mara kadhaa ndani ya wiki chache.

Ripoti hiyo inazungumzia pia usambazaji wa chanjo za corona usio na usawa unaomaanisha kwamba eneo la kusini mwa Afrika, ambalo lina idadi kubwa zaidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, ndilo pia lilipokea chanjo chache zaidi.

Barani Ulaya, idadi ya maambukizi, mapya ya VVU inapanda kwa asilimia 24, kwa mujibu wa mashirika hayo mawili ya afya.

Eneo lililofanyiwa utafiti linajumuisha mataifa 53, zikiwamo Israel, Urusi, Uturuki na Turkemistan, ripoti inasema kuna idadi kubwa ya watu walioambukizwa UKIMWI, bila kujijua na bado hawajapima. Kufikia mwaka jana 2020, katika mataifa 27 ya EU, pamoja na Iceland, Liechtenstein na Norway, kulikuwa tayari na watu 14,971 walioripotiwa kuambikizwa VVU, ambapo kwenye eneo zima la Ulaya, idadi ya wanaoishi na virusi hivyo ni 104,765.

Utafiti uliofanywa na mashirika hayo mawili ya afya umebaini kuwa kwenye mataifa mengi ya Ulaya Magharibi, maambukizo ya virusi vya UKIMWI husambazwa kupitia kujamiiana wanaume kwa wanaume bila kutumia kinga.

Katika mataifa ya Ulaya Mashariki, maambukizi husambazwa kupitia uchomaji sindano kwa watumiaji wa dawa za kulevya na pia ufanyaji mapenzi usiozingatia kinga.

Kiasi cha watu milioni 35 wameshafariki dunia kutokana na maradhi yanayoambatana na virusi vya UKIMWI tangu ugonjwa huo ugundulike mwaka 1984.

Umoja wa Mataifa (UN), ulikuwa umejiwekea lengo la kuutokomeza UKIMWI kufikia mwaka 2030, ulijikuta haukuweza kutimiza hata malengo yake ya ndani kufikia mwaka jana 2020.

Kwa mujibu wa Shirika la Kupambana na Ukimwi la Umoja wa Mataifa (UNAIDS), endapo programu za matibabu zitaendelea kwa viwango vya mwaka 2019, kutakuwa na ongezeko la vifo milioni 7.7 kutokana na UKIMWI kufikia mwaka 2030.

Kukiwa na fedha zaidi, shirika hilo linakadiria linaweza kuokoa maisha ya watu milioni 4.6 kati ya hao.

**DW**



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kupambana na Ukimwi la Umoja wa Mataifa (UNAIDS), Winnie Byanyima. Shirika hilo limesema kutakuwa na ongezeko la vifo milioni 7.7 kutokana na UKIMWI kufikia mwaka 2030. **PICHA: MAKTABA REUTERS**

# Polisi wa Sudan watumia gesi ya kutoa machozi kutawanya waandamanaji

**Khartoum,** SUDAN

MAOFISA wa usalama wa Sudan, wamelazimika kutumia gesi ya kutoa machozi, ili kudhibiti maelfu ya waandamanaji waliojitokeza kwenye barabara za mji mkuu Khartoum, ikiwa maandamano ya karibuni ya kupinga mapinduzi ya kijeshi ya mwezi uliopita.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AP, maandamano pia yalishuhudiwa kwenye miji mingine nchini humo.

Waziri mkuu aliyekuwa ameondolewa madarakani na jeshi wakati wa mapinduzi hayo, Abdalla Hamdock mapema mwezi huu alirejeshwa mamlakani, akiwa chini ya uangalizi wa kijeshi, hatua ambayo wanaharakati wa demokrasia wanaipinga.

Taifa hilo limeshuhudia maandamano makali tangu mapinduzi ya Oktoba 25, mwaka huu, kisha kukamatwa kwa zaidi ya maofisa 100 waliokuwa kwenye serikali ya kiraia.

Vikosi vya usalama vinasemekana kufanya msako mkali dhidi ya waandamanaji wakati watu 43 wakisemekana kufa tangu yalipoanza, kulingana na ripoti ya kamati ya madaktari inayofuatilia idadi ya maafa tangu maandamano yalipoanza nchini humo.

**VOA**

# Waziri Mkuu wa zamani Lesotho ashtakiwa madai mauaji mkewe

**Masru,** LESOTHO

WAZIRI Mkuu wa zamani wa Lesotho, Thomas Thabane ameshtakiwa kwa mauaji ya mke wake Lipolelo Thabane, mwaka 2017.

Mkewe wa sasa, Maesaiah, alishtakiwa kwa uhalifu kama huo mwaka jana.

Alikuwa akiishi na Thabane wakati wa mauaji hayo na wanatuhumiwa kuajiri watu waliotekeleza shambulizi hilo. wote wawili wamekana kuhusika.

Thabane alijiuzulu Mei 2020 kufuatia shinikizo la miezi kadhaa baada ya kutajwa kama mshukiwa.

Kesi hiyo imewashangaza wengi na kusababisha misukosuko ya kisiasa katika ufalme huo mdogo usio na bahari, ambao umezungukwa kabisa na Afrika Kusini.

Maesaiah Thabane, aliandamana na waziri mkuu huyo wa zamani mwenye umri wa miaka 82 hadi mahakamani. Alishtakiwa mwaka jana na kisha kuachiliwa kwa dhamana.

Mashtaka hayo yalisomwa katika ukumbi wa Mahakama Kuu katika mji mkuu wa Maseru, badala ya chumba cha Mahakama Kuu, jambo ambalo si la kawaida, shirika la habari la AFP liliripoti.

Watu wenye silaha walimpiga risasi na kumuua Lipolelo Thabane, Juni 14, mwaka 2017, siku mbili kabla ya Thabane kuapishwa kama waziri mkuu.

Alipokuwa akirudi nyumbani, aliviziwa, akapigwa risasi mara kadhaa akiwa karibu na kufa kando ya barabara. Alikuwa na umri wa miaka 58.

Wakati huo, Lipolelo alikuwa katikati ya kupata talaka kutoka kwa Thabane na alikuwa akiishi na mumewe tangu 2012.

Alihama na kuanza kuishi na Maesaiah kwa muda kati ya mwaka 2012 na 2017. Walioana miezi miwili baada ya kifo cha Lipolelo.

**BBC**

# 'NJE YA DIMBA NA STARS' USO KWA USO MASHABIKI MBEYA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI kabambe ya 'Nje ya Dimba na Stars' inayoendeshwa na bia ya Serengeti Lager, ambayo ni maalum kwa ajili ya kuhakikisha mashabiki wa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', wanafikiwa na wachezaji wa timu hiyo na kupata fursa ya kupiga nao stori na picha, sasa imewafikia wakazi wa jijini Mbeya.

Nje ya Dimba na Stars ambayo ni kampeni ya nchi nzima itakayodumu kwa miezi mitatu, ikilenga kuwapa nafasi mashabiki wa Taifa Stars kukutana na nyota wanaowapenda katika baa zao na pia kuwauliza maswali kuhusu maisha yao nje ya soka pamoja kupiga nao picha za ukumbusho, ilitua Mbeya jana na mashabiki kuitumia fursa hiyo kwa kupata nao chakula cha jioni.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Meneja Masoko wa Nyanda za Juu Kusini wa kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL), Denis Tairo, alisema bia ya Serengeti Lager ikiwa kama shabiki mkuu wa Taifa Stars, inajivunia kuwaletea mashabiki wa timu hiyo jijini Mbeya nyota wanaowapenda na kuwapa nafasi ya kuzungumza nao na hivyo kuwafahamu kwa undani zaidi.

"Shabiki mkuu na mdhamini wa timu yetu ya Taifa, Taifa Stars, bia ya Serengeti Lager, leo (jana), amewakutanisha mashabiki wa hapa Mbeya uso-kwa-uso na nyota ambao mara nyingi wamekuwa wakiwaona uwanjani. Hii ni fursa pekee ya mashabiki kujua maisha ya nyota wao nje ya uwanja," alisema.

Denis alisema kampeni hiyo ya nchi nzima itahusisha wachezaji wa Taifa Stars ambapo watatembelea mikoa ya Mbeya, Mwanza na Arusha na kukutana na mashabiki wao kupitia matukio kama pati za mwisho wa mwezi 'Nje ya Dimba na Stars'. Na kwenye matukio kama hayo mashabiki wataweza pia kujishindia zawadi mbalimbali na ofa za bia yao pendwa ya Serengeti Lager.

"Wachezaji watakuwa kwenye baa mbalimbali na wakati wateja wetu wa bia ya Serengeti Lager wakiendelea kuburudika na bia yao pendwa iliyotengenezwa kwa kimea kwa asilimia 100 na isiyoongezwa sukari, watapata nafasi ya kuwauliza maswali, kupiga picha na kupata sahihi zao," alisema

Aliwataka mashabiki wa Stars kutembelea kurasa za mitandao ya kijamii ya bia ya Serengeti Lager pamoja na kusikiliza redio kwa ajili ya kujua lini na wapi nyota wa Taifa Stars watakuwa.




Meneja Masoko wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Denis Tairo (katikati), akiwa na baadhi ya wachezaji wa Taifa Stars ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya 'Nje ya Dimba na Stars' ambapo wachezaji hao walikutana uso kwa uso na mashabiki wao wa mkoa wa Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtibwa sasa kurejea Manungu Complex

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kufungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC juzi kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi, huku ikiwa haijashinda mechi yoyote tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, timu ya Mtibwa Sugar imepata faraja, baada ya uwanja wake wa Manungu Complex kutarajiwa kukamilika Desemba 9, mwaka huu, hivyo kurejea tena kucheza dimba lake la nyumbani.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, amemwambia mwandishi wetu kuwa, uwanja huo ambao ulizuiwa kuchezwa mechi za Ligi Kuu kwa takriban misimu miwili sasa, unatarajiwa kukamilika Desemba 9, siku ya Uhuru wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara) na baada ya hapo watarejea kucheza uwanjani hapo.

"Uwanja wetu wa Manungu Complex uko kwenye hatua za mwisho kabisa, mpaka Desemba 9 tutaufungua, nitaita waandishi waje kuangalia. Ikumbukwe awali ulikuwa umezungushiwa mabati, lakini sasa hivi umezungushiwa ukuta, unajua hata hii kupoteza baadhi ya mechi inatokana na sisi kutokuwa na uwanja wa nyumbani, siku zote usipokuwa na nyumba maisha hayawi mazuri, ilikuwa mara leo uwanja wa Uhuru, kesho uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani kwa Masau Bwire, tulikuwa tunanyanyasika sana, lakini ujenzi umekamilika, nadhani tukirudi nyumbani tutaanza kushinda," alisema Kifaru.

Mbali na hilo, alisema kipindi hicho itakuwa pia imeshafanya mabadiliko kwenye idara yake ya ushambuliaji ambayo inaonekana kuwa butu, kwani kwenye mechi saba imefunga mabao mawili tu.

Mtibwa bado inaendelea kuburuza mkia kwenye msimamo wa ligi, ikiwa imecheza mechi saba, haijashinda, imepoteza michezo mitano na sare mbili, ikiwa na pointi mbili tu mpaka sasa.

## RC Mtwara: Nitashinda shindano kukuna nazi

**Na Abdallah Khamis, MTWARA**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amesema ana imani kubwa ataibuka mshindi katika mashindano ya kukuna nazi yanayotarajiwa kufanyika mkoani hapa kuanzia Desemba 3, mwaka huu ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru.

Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alitoa kauli hiyo jana mkoani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelezea maandalizi ya maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru kimkoa yatakayofanyika katika mji wa kitalii wa Mikindani

Alisema licha ya mshindani wake wa karibu, Katibu Tawala wa mkoa, Abdallah Malela, kujinadi kuwa ana aina zaidi ya tatu za ukunaji nazi, ni wazi atamuonyesha ubora wake katika shindano hilo baada ya kufanya mazoezi ya kutosha.

"Mwenzangu RAS Malela, amejinasibu kushinda na kunitajia aina mbalimbali ya tui atakalotoa, lakini mimi nitamshinda katika hili ingawa mchezaji bora hawezi kupatikana katika mchezo mmoja, hivyo nitamkaribisha tushindane na katika riadha pamoja na michezo ya kuogelea," alisema Gaguti

Alisema kuelekea siku hiyo, tayari mkoa wa Mtwara umeanza kushiriki shughuli mbalimbali ikiwamo mashindano ya insha kwa shule za msingi na sekondari, huku akieleza mbali na shindano la kukuna nazi, pia watakuwa na mashindano ya ngoma za asili, kuogelea na michezo maalumu kwa watu wenye mahitaji maalumu.

## Siboka aingia studio kufyatua 'Kisugugu'

**Na Sabato Kasika**

MSANII wa nyimbo za asili, Costa Siboka, ameingia studio kufyatua vibao viwili, ambavyo anatarajia kuvitambulisha rasmi kwenye tamasha la pasaka kisiwani Ukerewe, Mwanza.

Siboka ambaye pia ni kiongozi wa kundi la sanaa la Mfalme, amevitaja vibao hivyo kuwa ni 'Kisugugu' ambao umeimbwa kwa lugha ya kijita na 'Wawaa' Remix, ambazo alirekodi wiki iliyopita, jijini Dar es Salaam.

"Msimu wa Krismasi umewadia na kila mwaka huwa tunafanya tamasha liitwalo 'Shangwe za Ukerewe Festival', hivyo nitatumia nafasi hiyo kutambulisha nyimbo hizi mpya ambazo nimerekodi," alisema Siboka katika mahojiano maalumu na mwandishi wetu.

Amefafanua kuwa tamasha hilo litafanyika katika Uwanja wa Getrude Mongella na kwamba yeye ndiye mratibu ingawa pia atashiriki kutoa burudani akiwa na kundi lake la Mfalme.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MANCINI ATAJWA UNITED
KOCHA Mkuu wa Italia na kwa zamani wa Manchester City, Roberto Mancini ameibuka kuwa mgombea wa kuteuliwa kuwa kocha wa Manchester United msimu ujao wa majira ya joto. **(Telegraph)**

### COUTINHO SASA SOKONI
BARCELONA wameipa Manchester United fursa ya kumsajili winga wa Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 29. **(Sport)**

### RUDIGER KUTUA MADRID
REAL Madrid wana matumaini kuhusu nafasi yao ya kumsajili beki wa kati wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28.**(Goal)**

### TORRES AKARIBIA BARCA
BARCELONA wana "makubaliano kamili" ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na Hispania, Ferran Torres, mwenye umri wa miaka 21, lakini wanatumai watapunguziwa bei wanayohitaji ya pauni milioni 60. **(Sport)**

### CHELSEA, LIVER KWA ARAUJO
CHELSEA na Liverpool zote zinatarajia kumsajili mlinzi wa Barcelona na Uruguay mwenye umri wa miaka 22, Ronald Araujo.**(Sport)**

### BERGWIJN AWINDWA AJAX
AJAX wanataka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Tottenham na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24. **(De Telegraaf)**

### BARBOSA KURUDI ULAYA
MSHAMBULIAJI wa Flamengo na Brazil, Gabriel Barbosa anataka kurejea Ulaya huku Arsenal, West Ham na Newcastle wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ambaye aliwahi kuchezea Inter Milan na Benfica. **(90min)**

### TCHOUAMENI ANUKIA CHELSEA
CHELSEA wamepata nyongeza ya uhamisho huku Juventus wakiwa wamejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Monaco na Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21. **(Calciomercato)**

### TRAORE APUNGUZWA BEI
KLABU ya Wolves inajiandaa kupunguza bei ya winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25 kwa pauni milioni 32. **(Football Insider)**

### MAHREZ NA MKATABA MPYA
MANCHESTER City wameongeza juhudi zao za kutaka kumwongezea mkataba mpya, Mualgeria Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 30, ambaye amebakiwa na miezi 18 katika mkataba wake wa sasa. **(Sun)**

### TARKOWSKI HATARUHUSIWA JANUARI
KLABU ya Burnley haitamruhusu mlinzi wa England, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 29 kuondoka Januari.**(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: SISHINDANI NA MESSI TUZO BALLON D'OR

Napigania kushinda kwa ajili yangu binafsi na kwa wale wanaonipenda, sipiganii kushinda dhidi ya mtu mwingine...

**LONDON, England**

CRISTIANO Ronaldo amemshutumu mhariri mmoja wa soka nchini Ufaransa kwa kudanganya baada ya kusema kwamba, lengo la raia huyo wa Ureno ni kustaafu akiwa na tuzo nyingi za Ballon d'Or zaidi ya Lionel Messi.

Mwandaaji wa tuzo ya Ballon d'Or, Pascal Ferre, alitoa madai hayo kwenye gazeti la New York Times.

Mshambuliaji wa PSG, Messi alishinda tuzo yake ya saba Jumatatu huku mshindi mara tano, Ronaldo akimaliza katika nafasi ya sita.

"Mimi hushinda tuzo ya Ballon d'Or kwanza kibinafsi na pili kwa klabu ninayoichezea," alisema Ronaldo akinukuliwa na Daily Mail.

"Napigania kushinda taji hilo kwangu mimi binafsi na kwa wale wanaonipenda, sipiganii kushinda dhidi ya mtu mwingine.

"Siku ya Ijumaa, Ferre aliliambia New York Times: Ronaldo ana lengo moja tu, na hilo ni kustaafu na tuzo nyingi zaidi za Ballon d'Or zaidi ya Messi - na najua hilo kwa sababu ameniambia."

Ronaldo alijibu katika mtandao wa kijamii akisema: Pascal Ferre alidanganya, alitumia jina langu kujikuza na kukuza gazeti analolifanyia kazi.

"Haikubaliki kwamba mtu anayehusika kutoa tuzo muhimu kama hiyo anaweza kudanganya kwa njia kama hiyo, hakika ni kumkosea heshima mtu ambaye ameheshimu soka la Ufaransa na tuzo ya Ballon d'Or.

Ballon d'Or - ni tuzo anayopatiwa mchezaji bora wa soka wa mwaka - hupigiwa kura na waandishi 180 kote duniani.

Messi alikuwa ameshinda tuzo hiyo mara nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote, baada ya kuibuka mshindi mwaka 2009, 2010, 2011, 2012, 2015 na 2019.

Ronaldo, ambaye mara ya mwisho alishinda tuzo hiyo mwaka 2017, alimaliza nje ya wachezaji watano bora duniani kwa mara ya kwanza tangu 2010.

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
2.06 | 3.53 | 3.43
ARSENAL

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 735



# KLOPP ATOA NENO TUZO BALLOD D'OR

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amehoji matokeo ya tuzo ya Ballon d'Or 2021 na amesema Robert Lewandowski na Mohamed Salah hawakutendewa haki baada ya Lionel Messi kutwaa tuzo hiyo kwa mara ya saba.

Tuzo hiyo inayotolewa na Jarida la Ufaransa, France Football na kupigiwa kura na waandishi wa habari waliochaguliwa duniani kote, haikufanyika mwaka jana kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Mshambuliaji wa Bayern Munich, Lewandowski alimaliza nafasi ya pili huku Salah wa Liverpool akimaliza nafasi ya saba.

Kocha wa Liverpool, Klopp ameibuka na kusema kuwa Messi amependelewa dhidi ya Lewandowski na Salah.

"Sina uhakika kwa asilimia 100 kuhusu tuzo ya Ballon d'Or," alisema Klopp wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

"Mara zote anapewa Messi na sina tatizo na hilo, lakini kama huwezi kumpa Robert Lewandowski wakati huu baada ya kuwa na mwaka bora, kwa hakika kabisa inashangaza.

"Na Mo (Salah) alitakiwa kuwa kwenye nafasi ya juu zaidi. Ilishangaza na nafasi aliyokuwapo.

"Niliona kura sehemu moja, sijui namna gani wanapiga hizo kura. Ni waandishi wa habari, sidhani, sina uhakika sana kwa hilo."



# Lukaku ataleta mchango mkubwa atamba Tuchel

**LONDON, England**

THOMAS Tuchel anaamini kwamba, Romelu Lukaku ataleta mchango mkubwa kwa Chelsea wakati akirudi kutoka chumba cha majeruhi, lakini amesisitiza 'Blues' hao lazima wawe wavumilivu kuhusu straika huyo.

Lukaku aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi katika klabu hiyo, amefunga mabao manne katika mechi 12 tangu aliporudi kwa mara ya pili pale Stamford Bridge akitokea Inter Milan.

Lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ublegiji alikosekana dimbani mwezi uliopita kutokana na kuumia kifundo cha mguu.

Aliingia akitokea benchi wikiendi iliyopita wakati Chelsea ikitoka sare na Manchester United na jana Jumatano alitarajia kuanza dhidi ya Watford

Tuchel hana shaka na ubora wa Lukaku na anaamini atakuwa na mchango mkubwa kwa Blues hao wakati atakaporudi kamili uwanjani.

Lakini kocha huyo amesisitiza, kunahitajika uvumilivu kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Tumeonyesha ubora tukiwa na yeye na pia tumekuwa bora bila uwapo wake na tumeweza kuwa na uwezo wa kufunga na kushinda," amesema Tuchel.

"Nafikiri tupo kwenye hatua ya kuzoea njia zote, jambo la msingi ni kwamba, tunatakiwa kuwa wavumilivu kuhusu yeye."

# 5,865,580

# JACKPOT MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/12/21 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 02. 04/12/21 | 18:00 | Reading vs Hull City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 03. 04/12/21 | 18:00 | Bristol City vs Derby | 2.40 | 3.14 | 2.89 |
| 04. 04/12/21 | 18:00 | Barnsley vs Huddersfield | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 05. 04/12/21 | 18:00 | Newcastle vs Burnley | 2.24 | 3.31 | 3.21 |
| 06. 04/12/21 | 18:00 | Southampton vs Brighton | 2.42 | 3.30 | 2.90 |
| 07. 04/12/21 | 23:00 | Real Sociedad vs Real Madrid | 3.01 | 3.26 | 2.37 |
| 08. 05/12/21 | 14:30 | Bologna vs Fiorentina | 2.56 | 3.51 | 2.61 |
| 09. 05/12/21 | 16:00 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.30 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/12/21 | 17:00 | Lorient vs Nantes | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 11. 05/12/21 | 17:30 | QPR vs Stoke City | 2.36 | 3.23 | 2.89 |
| 12. 05/12/21 | 19:30 | Aston Villa vs Leicester | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 13. 05/12/21 | 20:30 | Levante vs Osasuna | 2.45 | 3.20 | 2.95 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 02 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:45 | 4162 | CSKA 1948 vs Pirin Blagoevgrad | 1.58 | 3.87 | 4.83 |
| 14:00 | 2618 | Pars Jonoubi Jam vs Shahrdari Hamedan | 3.17 | 2.60 | 2.50 |
| 15:00 | 1622 | FK Arsenal Tivat vs Jedinstvo BP | 2.60 | 2.90 | 3.00 |
| 15:00 | 2456 | Novi Pazar vs Backa Palanka | 1.58 | 3.75 | 5.00 |
| 15:00 | 2532 | OFK Titograd vs Bokelj | 8.80 | 4.00 | 1.43 |
| 15:00 | 3371 | Berane vs FK Cetinje | 1.69 | 3.23 | 5.02 |
| 15:00 | 4055 | OFK Igalo 1929 vs Mladost DG | 1.98 | 2.93 | 3.94 |
| 16:00 | 1617 | Al Gharafa SC vs Al Arabi Doha SC | 2.66 | 3.43 | 2.32 |
| 16:00 | 3817 | Ludogorets Razgrad vs Arda Kurdzhali | 1.28 | 5.01 | 8.29 |
| 16:00 | 5551 | Nikolaos vs Anagennisi Karditsas | 4.25 | 3.28 | 1.79 |
| 16:30 | 1466 | Persela Lamongan vs PSM Makassar | 4.54 | 3.86 | 1.61 |
| 17:00 | 1214 | Jamshedpur vs Hyderabad FC | 2.64 | 3.27 | 2.40 |
| 17:00 | 5881 | Javor Ivanjica vs Vojvodina | 3.65 | 3.12 | 1.98 |
| 17:20 | 3507 | Al Shabab Kuwait vs Al Fehaheel | 2.45 | 3.51 | 2.45 |
| 18:00 | 3002 | Velez CF vs Las Palmas UD | 9.87 | 6.12 | 1.23 |
| 18:00 | 4027 | Lamia vs Ionikos Nikea FC | 2.17 | 2.95 | 3.33 |
| 18:10 | 4591 | Al Khoor vs Al-Sailiya SC | 2.80 | 3.43 | 2.22 |
| 18:30 | 4011 | CSKA Sofia vs Lokomotive Sofia | 1.24 | 5.00 | 10.58 |
| 19:35 | 3852 | AL Nasr vs Kazma SC | 3.08 | 3.42 | 2.07 |
| 20:00 | 4309 | Cruz Azul U20 vs Santos Laguna U20 | 2.74 | 2.98 | 2.50 |
| 20:30 | 1407 | Torino vs Empoli | 1.76 | 3.79 | 4.39 |
| 20:30 | 2012 | Hvidovre IF vs Esbjerg | 1.72 | 3.75 | 3.95 |
| 20:30 | 5929 | Orlando Pirates vs Baroka FC | 1.58 | 3.67 | 5.67 |
| 20:45 | 2666 | AZ Alkmaar vs Fortuna Sittard | 1.27 | 5.51 | 9.05 |
| 21:00 | 2072 | Dalkurd FF vs Gais | 2.51 | 3.51 | 2.66 |
| 21:00 | 3233 | Skovde Aik vs Akropolis IF | 2.70 | 3.45 | 2.50 |
| 21:00 | 4557 | Guijuelo vs Rayo Vallecano | 22.64 | 15.75 | 1.03 |
| 21:00 | 5348 | SD Gernika vs Eibar | 9.86 | 6.71 | 1.21 |
| 21:30 | 1548 | Acso Filiasi vs Universitatea Craiova | 25.93 | 9.41 | 1.05 |
| 21:30 | 1782 | Pena Sport FC vs Malaga | 8.05 | 5.10 | 1.32 |
| 21:30 | 2684 | Maccabi Haifa vs Hapoel Haifa | 1.43 | 4.14 | 6.36 |
| 21:30 | 4255 | ASC 09 Dortmund vs TUS Haltern | 1.45 | 5.40 | 5.40 |
| 22:00 | 2969 | Guabira Montero vs Royal Pari Sion | 2.01 | 3.47 | 3.18 |
| 22:00 | 3489 | Leioa vs Elche | 29.58 | 11.83 | 1.05 |
| 22:00 | 3915 | CD Cristo Atletico vs Real Union Irun | 6.10 | 4.13 | 1.49 |
| 22:00 | 4080 | Real Potosi vs Independiente Petrolero | 2.74 | 3.51 | 2.22 |
| 22:00 | 4515 | Charleroi U21 vs Antwerp U21 | 1.45 | 4.74 | 5.03 |
| 22:00 | 4757 | UD Llanera vs UD Logrones | 10.88 | 5.74 | 1.24 |
| 22:00 | 4891 | Atletico Pulpileno vs CD Castellon | 5.35 | 3.96 | 1.57 |
| 22:00 | 5338 | Widzew Lodz vs Wisla Krakow | 2.88 | 3.26 | 2.24 |
| 22:15 | 1887 | AD Union Adarve vs Lugo | 7.11 | 4.74 | 1.38 |
| 22:30 | 2817 | Tottenham vs Brentford | 1.63 | 3.95 | 5.20 |
| 22:30 | 4892 | CD Eldense vs Rayo Majadahonda | 5.11 | 3.93 | 1.60 |
| 22:45 | 1206 | Celtic vs Hearts | 1.38 | 4.82 | 7.08 |
| 22:45 | 3197 | Standard Liege vs Kfco Wilrijk | 1.70 | 3.71 | 4.40 |
| 22:45 | 5720 | Lazio vs Udinese | 1.65 | 4.01 | 4.92 |
| 23:00 | 1290 | CD Ibiza Islas Pitiusas vs Tenerife | 9.86 | 5.52 | 1.26 |
| 23:00 | 5963 | Ajax vs Willem II Tilburg | 1.06 | 10.78 | 23.52 |
| 23:15 | 3156 | Manchester Utd vs Arsenal | 2.06 | 3.53 | 3.43 |
| 23:15 | 5589 | Casa Pia Atletico vs Varzim | 1.46 | 4.20 | 6.25 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TABORA WAPAGAWA KMC KUIPELEKA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

VIONGOZI wa soka mkoani Tabora na mashabiki kandanda, wameonyesha kufurahia mechi ya Ligi Kuu kati ya KMC na Simba kupelekwa uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani humo, na katika hili wamesema tayari wameshaanza maandalizi kabambe kwa ajili ya kupokea wageni hao na kuimarisha usalama.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Tabora, Yusuph Kitumbo, amesema baada ya kupata taarifa ya kupelekwa mechi kwenye Uwanja huo, inayotarajiwa kuchezwa Desemba 24, mwaka huu, mashabiki wa soka mkoani Tabora wameonekana kufurahi na kuanza maandalizi ya kuishuhudia mechi hiyo, huku mabishano yakitawala kila kona.

Novemba 29, Bodi ya Ligi ilitoa taarifa kuwa mchezo namba 78, kati ya KMC dhidi ya Simba umehamishwa toka Uwanja wa Uhuru ulipopangwa kuchezwa awali na kupelekwa kwenye uwanja huo uliopo mkoani Tabora.

"Tumeshaanza maandalizi, uwanja wetu ni mzuri na tayari tulishaanza ukarabati huko nyuma, kama utakumbuka Yanga ilicheza na Biashara United hapa na tumeendelea kuutunza uwanja, kwa hiyo baada ya kupata taarifa hiyo, tumeanza tena kuuangalia pale ambapo kutahitaji marekebisho, pamoja na kuuweka kwenye hali nzuri hasa sehemu ya kuchezea, lakini pia kwenye majukwaa," alisema Kitumbo.

Alisema tayari chama chao kimeanza mazungumzo na serikali ya mkoa, ili kuangalia namna ya kupokea wageni kutoka mikoa tofauti, pamoja na ulinzi kwa mashabiki watakaofika kuangalia mechi hiyo.

Hii itakuwa ni mara ya pili kwa wakazi wa mkoa huo kutazama timu kubwa zenye mashabiki wengi, kwani Juni 25, mwaka huu, walishuhuda mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA kati ya Yanga na Biashara United, iliyoisha kwa Yanga kushinda bao 1-0.



# Omog yupo sana Mtibwa Sugar

**Na Dennis Fussi**

LICHA ya matokeo mabaya inayopata Mtibwa Sugar kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Joseph Omog, ataendelea kukinoa kikosi hicho, kwa mujibu wa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru.

Mtibwa juzi ilifungwa bao 1-0 na Azam FC kwenye mchezo wake wa saba wa Ligi Kuu msimu huu, na inaendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi mbili baada ya kupoteza mechi tano na kutoka sare mbili.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Kifaru alisema wapo kwenye wakati mgumu, lakini bado wana imani na kocha wao, Omog kuendelea kuliongoza Jahazi hilo.



"Tuna mkataba na Joseph Omog wa miaka miwili, hivyo tutaendelea kuwa naye, tunaamini huu ni upepo mbaya tu na utapita na hali itakuwa sawa tu," alisema Kifaru.

Alisema wanaamini uwezo wa Omog ambaye aliwahi kuzinoa Simba na Azam FC kwa nyakati tofauti.

"Omog ni kocha mkubwa na mwenye rekodi za aina yake. Kumbuka yeye ndiye alikuwa kocha mzawa pekee wakati anaiongoza nchi yake Cameroon kwenye michuano ya Afcon iliyopita hivyo tuna imani naye," alisema.

Wakati huo huo, Kifaru amesema kuwa kwa sasa uwanja wao umefikia asilimia 80 ya maboresho na hivyo anaamini pengine mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu wanaweza kucheza katika uwanja wao wa nyumbani kama ukifunguliwa.

Uwanja huo ulifungiwa na bodi ya ligi nchini (TPLB) ili kufanyiwa maboresho zaidi.

UKURASA 21

# Michezo

Alhamisi Desemba 2, 2021

Nipashe



Ronaldo: Sishindani na Messi tuzo Ballon d'Or

HUNIWEZI...




Mshambuliaji hatari wa Timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania kwa Watu wenye Ulemavu 'Tembo Warriors', Franck Ngairo, akimtoka beki wa Cameroon, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 5-0 kwenye mechi hiyo ya Kombe la Mataifa ya Afrika (CANAF), iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YALIA NA RATIBA, YANGA SIRI YA MABAO

●●● Yakiri Desemba kuielemea, lakini yasema acha kazi iendelee wamalizane na Red Arrows kwanza...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI jana ikicheza mchezo wa kwanza mwezi huu, Simba imeeleza inakabiliwa na ratiba ngumu katika kipindi hiki cha Desemba, ikitakiwa kucheza michezo sita ukiwamo mmoja wa kimataifa; Kombe la Shirikisho Afrika na mmoja wa Kombe la FA, lakini upande wa watani zao, Yanga wametoa siri ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya Kwanza juzi.

Ratiba inayoelezwa kuwa ngumu kwa Simba ilianza jana kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Geita Gold FC uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Desemba 5, itacheza mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows nchini Zambia.

Baada ya mchezo huo, Simba itarejea nyumbani kucheza dhidi ya Yanga Desemba 11 na kisha siku nne baadaye kuvaana na JKT Tanzania kwenye mechi ya Kombe la FA kabla ya Desemba 18 kuifuata Kagera Sugar ikiwa ni siku sita kabla ya kwenda mkoani Tabora kuvaana na KMC FC, ambayo imehamishia mechi yake hiyo Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, akizungumza na gazeti hili, alikiri kuwa ratiba imewabana, lakini hawana namna zaidi ya kupambana ili kufanya vizuri.

"Ratiba kweli imetubana kwa mwezi huu, ukiangalia baada ya mchezo wa leo (jana) tutatakiwa kusafiri kwenda Zambia kuuwahi mchezo wa marudiano dhidi ya Red Arrows, lakini ni lazima tutapambane na kujiandaa kuweza kukabiliana na ratiba hii na hapo hapo kuhakikisha timu inafanya vizuri," alisema Matola.

Aidha, alisema Kocha Mkuu, Pablo Franco, ameiona ratiba na anaandaa programu ya kukabiliana nayo huku kipaumbele chake kikiwa ni timu kufanya vizuri kwenye mchezo hiyo.

Hata hivyo, wakati Simba ikieleza hayo, watani zao Yanga wamesema ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya Kwanza juzi kwenye Uwanja wsa Sokoine jijini Mbeya ulikuwa ni mpango makakati wao kutokana na hali ya Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, akizungumza baada ya mechi kumalizika, alisema mchezo haukuwa rahisi hata kidogo kutokana na kwamba walicheza na timu yenye vijana wengi na wenye kujituma, hivyo mpango wao ulikuwa ni kupata mabao ya mapema ili kuufanya mchezo uwe rahisi kwao.

"Tulijua utakuwa mgumu, lakini sisi tulijiandaa kucheza na timu nzuri, yenye vijana wenye kujituma na kwa sababu kiwanja hakikuwa rafiki, tuliamua kufutafuta mabao ya mapema ili kuufanya mchezo kuwa mwepesi kwetu na mgumu kwa wapinzani na ndiyo lilikuwa lengo letu kubwa," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Alisema ushindi huo unawapa ari zaidi na kujiamini kwenda kuweka mipango ya kujiandaa na mechi inayofuata.

Yanga inajiandaa na mechi ya watani zao wa jadi, Simba, itakayochezwa Desemba 11, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa upande wa Mbeya Kwanza, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Haruna Hererimana, alisema wamekubali kupoteza mechi hiyo kutokana na wachezaji wake kutokuwa makini kwenye ukabaji, hasa kipindi cha kwanza.

"Tumecheza vizuri, na Yanga wamecheza vizuri, wenzetu ni wazoefu kwa hiyo walikuwa wanatumia makosa yetu kwa sababu hatukuwa makini kwenye ukabaji, tukipoteza mpira wenyewe wanapiga juu pembeni, mabeki wetu na mawinga wakawa wanachelewa kwenda kuziba nafasi mapema, hii ilitupa shida sana hasa kipindi cha kwanza, kidogo tuliziba mianya kipindi cha pili," alisema kocha huyo ambaye ni Mrundi.

## Ngairo aipeleka Tembo Warriors Kombe la Dunia

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania kwa Watu wenye Ulemavu 'Tembo Warriors', Franck Ngairo, amekuwa mwiba mkali kwa timu pinzani wakati akitoa mchango mkubwa kwa kuiwezesha kufuzu kucheza fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Uturuki.

Ngairo ambaye juzi aliipeleka Tembo Warriors hatua ya robo fainali baada ya kuifungia bao pekee wakati ikishindi 1-0 dhidi ya Sierra Leone, jana aliendeleza moto wake wa kucheka na nyavu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuiwezesha timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Cameroon, hivyo kufuzu hatua ya nusu fainali, ambayo imewapa tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia mwakani.

Timu nne zilizofuzu hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya Afrika kwa watu wenye ulemavu (CANAF), inayofanyika hapa nchini, zimefuzu moja kwa moja kushiriki fainali za Kombe la Dunia nchini Uturuki na hadi gazeti hili linakwenda mitamboni zilizokuwa zimeshafuzu ni Tanzania na Ghana.

Mabao ya Tembo Warriors katika mchezo huo dhidi ya Cameroon, yalifungwa na Alfan Kiyanga dakika ya pili na 15, Ramadhan Chomelo dakika ya 18 kabla ya Ngairo kuhitimisha shughuli hiyo dakika ya 36 na 44.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana baada ya mchezo huo, Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema Tanzania ni mara yake ya kwanza kwenda kucheza Kombe la Dunia na timu ya Tembo Warriors ambao ni wenye ulemavu wa viungo, wameliheshimisha taifa katika anga za kimataifa, hivyo atatoa zawadi ya Sh. 200,000 kwa kila mchezaji kutoka mfukoni kwake kutokana na kutambua kazi kubwa waliyoifanya.

"Kwa mara ya kwanza Tanzania itacheza Kombe la Dunia, si haba kuingia huku kupitia soka la walemavu, Tembo Warriors wametupa soka na changamoto kwetu na timu zetu zingine za taifa, kwa wachezaji waliokamilika viungo kuelekea michuano ya kimataifa," alisema Bashungwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042